SUPA JACKPOT
TZS.1,096,041,286
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 3

**UWEKEZAJI** wa viwanda PSSSF kutoa ajira 1,300




UKURASA 11


# Nipashe

Jumamosi Aprili 1, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581267

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Watu 300 wadai kuibiwa bil. 16/-

**YUMO** Mchungaji KKKT, alitoa neno, mstaafu alambwa mil. 300/- za mafao ...

*Endelea ukurasa wa 2*



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akiwa na mkewe, Mbonimpaye Mpango, wakimuaga Makamu wa Rais wa Marekani, Kamala Harris na mumewe, Douglas Emhoff, kabla ya kuondoka katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), Dar es Salaam jana, baada ya kuhitimisha ziara nchini. **PICHA: OMR**

## JK: Baadhi ya sheria zimepitwa na wakati, zifanyiwe mabadiliko

UKURASA 2



Rais mstaafu, Dk. Jakaya Kikwete, akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutoa maoni yake mbele ya Tume ya Kuboresha Mifumo ya Haki Jinai, Dar es Salaam jana. **PICHA: RESTUTA JAMES**



UKURASA WA 3

### JAJI KIONGOZI ATUPIA JICHO MASHAURI YA MUDA MREFU

JAJI Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mustapher Siyani, amewaagiza maofisa wa mahakama, wakiwamo majaji...

UKURASA WA 4

### MRADI WA BILIONI 119/- KUPUNGUZA KIU YA MAJI RUANGWA, NACHINGWEA

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa amesema serikali imeandaa mradi mkubwa wa maji wenye thamani...

UKURASA WA 5

### ULEGA ANADI FURSA MIFUGO, UVUVI UGHAIBUNI

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amekutana na wadau wa maendeleo kutoka taasisi na kampuni mbalimbali Italia na...

## Makandarasi 500 wafutiwa usajili kwa kukosa sifa, kukiuka maadili

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA YAAHIDI FURAHA CONGO UK. 24 **KATUNI** UK. 6



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akizungumza na Rais mstaafu wa Zanzibar, Dk. Salmin Amour Juma, alipofika nyumbani kwake Migombani Wilaya ya Mjini Unguja, jijini Zanzibar jana, kwa ajili ya kumsalimia na kumjulia hali. **PICHA: IKULU**

# Watu 300 wadai kuibiwa bil. 16/-

**Na Mary Kadoke**

ZAIDI ya Watanzania 300, akiwamo Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mashariki na Pwani (DMP), Joseph Maseghe, wamedaiwa kutapeliwa zaidi ya Sh. Bilioni 16 walizokuwa wamewekeza kupitia kampuni ya BestWay Capital Management (BCM) Limited.

Baadhi ya wawekezaji hao, kwa niaba ya wenzao, waliwasilisha madai hayo jana katika mkutano na waandishi wa habari, uliofanyika Dar es Salaam.

Charles Kapongo, mmoja wa wawekezaji wa kampuni hiyo, alisema alifikia uamuzi wa kuwekeza pesa zake BCM mwaka 2020 baada ya kujiridhisha uhalali na utendaji kazi wa kampuni hiyo katika mamlaka mbalimbali.

"Nilikuwa mwekezaji katika kampuni ya BestWay Capital Management Limited (BCM) tangu mwaka 2020. Kabla ya kufikia hatua ya kuwekeza, awali nilifanya jitihada binafsi na kujiridhisha na kuhakikisha walikuwa wanafanya kazi kihalali. Mimi pamoja na mke wangu, tumepoteza Sh. milioni 100," alisema Kapongo.

Alisema moja ya masharti katika uwekezaji kwenye kampuni hiyo ilikuwa kuwekeza si chini ya Sh. milioni 23, kufungua akaunti pamoja na kujaza fomu, baada ya kutimiza masharti hayo, mhusika alipata mkataba wa mwaka au miaka miwili na kupewa asilimia sita ya pesa aliyokuwa amewekeza kama faida waliyokuwa wanalipwa kila mwezi.

Licha ya kuwepo kwa utaratibu huo, alisema Mkurugenzi wa Mtendaji wa BCM, Steven Ndaula, raia wa Tanzania, alibadilisha mfumo wa malipo na kuanzisha mfumo mbadala wa malipo, maarufu kama 'wallet payment'.

"Baada ya mfumo mpya wa malipo kuanzishwa ndipo changamoto zilipoanza, tumejaribu kuandika barua kama 10 kwa Wizara ya Mambo ya Ndani (ya Nchi) na kulihusisha Jeshi la Polisi lakini harakati zimekuwa zikiishia njiani," alisema.

Kwa mujibu wa Kapongo, Ndaula kwa sasa ni mwekezaji katika mji wa Dubai na kwamba licha ya kufanya mazungumzo na bodi ya wakurugenzi ili kutoa msaada wa nini kifanyike, mwisho wake haukuwa na majibu.

"Tunaomba Bwana Steven aje nchini tunajua yuko Dubai. Tunaomba pia Rais Samia Suluhu Hassan achukue jitihada za kusaidia maana asilimia 80 ya wawekezaji ni wazee na miongoni wako serikalini," alisema.

Joseph Missana, mwekezaji mwingine katika kampuni hiyo, alisema alijiridhisha na uhalali wa utendaji kazi wa kampuni (BCM) na kuamua kuwekeza Sh. milioni 300 alizokuwa amelipwa kama mafao.

"Baada ya kustaafu nilitaka nipate sehemu ya kuwekeza ili nipate faida. Katika kutafakari, ikaja BCM niliyohakikishiwa na kujiridhisha kuwa ilikuwa sehemu salama ya kuwekeza pesa zangu maana ilikuwa imesajiliwa na walikuwa wanalipa kodi ikiwamo 'withholding tax' (kodi ya zuio) Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)," alisema.

Missana alisema anakumbuka baada ya kuwekeza fedha hizo, alilipwa Sh. milioni 30 katika awamu ya kwanza na Sh. milioni 14 awamu ya pili ndani ya miezi sita baada ya kujiunga. Alisema baada ya hapo, mambo yalianza kwenda kombo baada ya kutafuta kila njia kukutana na Ndaula bila mafanikio.

Kutokana na kukumbwa na mkasa huo, Missana aliiomba serikali kuingilia kati kutokana na kuwepo kwa vielelezo vya uhalali wa utendaji kazi wa BCM pamoja na jitihada zilizofanywa awali za kupeleka malalamiko Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Agosti, mwaka jana lakini mpaka sasa bado haijatoa tamko lolote.

Mchungaji Maseghe, ambaye ametajwa kuwa alikuwa mmoja wa wakurugenzi katika kampuni hiyo, alikataa kuwa alikuwa na wadhifa huo licha ya kukiri kwamba jina lake liliandikwa tu.

"Hiyo ni kampuni ya kitapeli tu haipo. Mimi siyo mkurugenzi, niliandikwa tu walitumia 'profile' (wasifu) yangu (wangu). Niliwekeza Sh. milioni 200 ambazo nimepoteza," alisema Mchungaji Maseghe ambaye alikuwa anamiliki hisa 139.

Kutokana na mkasa huo, Mchungaji Maseghe aliwataka Watanzania kutokudanganywa kirahisi na wizi huo unaoendelea nchini na kuwaomba wapeleke fedha zao katika mifuko iliyohalalishwa kama UTT AMIS na kwenye hatifungani za serikali au benki zinazotambulika.

KAULI YA MKURUGENZI

Badaye, Ndaula alipotafutwa, kwa ujumbe mfupi wa WhatsApp kwamba: "Please share the names and contacts of those people complaining to the media. Then I will answer them for any information required. Otherwise, I am communicating with my clients throughout. They know what is going on all my stakeholders."

Kwa tafsiri isiyo rasmi ya Kiswahili alimaanisha; " Tafadhali Naomba unitumie majina na namba za hao watu wanaolalamika kupitia vyombo vya habari ili nijibu hoja zao. Vinginevyo, ninawasiliana na wateja na wanajua kinachoendelea kwa wadau wangu."

**YALIYOTOKEA AWALI**

Madai ya watu kutapeliwa kupitia kampuni kama hiyo, yaliwahi kufanywa na kampuni ya upatu ya Development Entrepreneurship for Community Initiative (DECI) mwaka 2009 na kwamba Watanzania wengi walipoteza mamilioni ya shilingi kwa kile kilichodaiwa 'kupanda mbegu na kuvuna'.

Pia kampuni ya Mr. Kuku ambaye alikuwa akiendesha biashara ya upatu na kupokea miamala ya fedha bila ya kuwa na leseni, alisababisha Watanzania kuingia katika mkumbo wa kuibiwa fedha. Pia wengine waliiwa fedha zao kupitia kampuni ya Idea Debater kwa lengo la kuvuna fedha na kujikuta wakiambulia machungu.

# JK: Baadhi ya sheria zimepitwa na wakati, zifutwe, zibadilishwe

**Na Restuta James**

RAIS Mstaafu, Dk. Jakaya Kikwete, amependekeza baadhi ya sheria nchini zifutwe na zingine zifanyiwe maboresho ili kuendana na mazingira ya sasa.

Kadhalika, amependekeza vyombo vinavyosimamia utoaji wa haki ikiwamo Jeshi la Polisi, Mamlaka ya Kudhibiti, Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mahakama na Magereza, vitathminiwe na kufanyiwa maboresho yanayokidhi hali ya sasa.

Aliyasema hayo jana Dar es Salaam baada ya kutoa maoni katika Tume ya Kuboresha Mifumo ya Haki Jinai inayoongozwa na Jaji Mkuu Mstaafu, Othman Mohamed Chande.

"Ziko sheria nyingine zinahitaji kuboreshwa, zipo nyingine zinazohitaji kutokuwepo, hao (Tume), ndiyo watakaoangalia sheria ipi, kwa sababu ipi ifanyiwe marekebisho," alisema.

Bila kuzungumzia kwa undani, alisema kuna haja ya kutazama mfumo wa vyombo vinavyoshughulikia mfumo wa haki na kupima penye madhaifu ili paboreshwe na panapofanya vizuri paongezwe nguvu zaidi.

"Mambo yanakwenda, lakini siyo vibaya kuboresha kile kinachofanyika sasa hivi. Kwanza, nimpongeze Rais (Samia Suluhu Hassan), ameteua watu ambao ni 'competent' (wenye uwezo), ambao watatoa ushauri makini kwa sababu ni watu ambao wanauzoefu," alisema Dk. Kikwete.

Dk. Kikwete ambaye alitumia takribani saa mbili kutoa maoni yake mbele ya tume, alisema mfumo huo unapaswa kuangaliwa kuanzia kwenye sheria hasa vyombo vinavyozuia na kushughulikia wahalifu kama polisi, TAKUKURU, DCEA hadi Mahakama na Magereza.

"Kuna haja ya kutazama vyombo hivi hao tume ndiyo wana kazi maana wanasikiliza maoni ya wengi, wanaenda wanapima," alisema.

Alisema ametoa maoni kwa kuzingatia uzoefu wake wa urais, akieleza kuwa tume ina uhuru wa kuzingatia au kuacha maoni yake kwa manufaa ya nchi.

"Nimeangalia mifumo ya taasisi hizi na nimezungumza zaidi kwa uzoefu wangu nilivyokuwa rais, nilivyoshughulikia vyombo hivi na ninavyoona mazingira yalivyo sasa ni eneo gani nadhani wanaweza kuimarisha zaidi na waliimarishe vipi. Wao ndio watakaoamua yale waliyoyasikia kwangu na kwa mwingine na hatimaye wapendekeze kwa rais," alisema.

Alisema ana imani kwamba tume ya Jaji Chande itatoa mapendekezo mazuri yatakayoimarisha mifumo ya haki jinai, likiwamo jeshi la polisi.

"Tume itaangalia kwa upana wake mambo yalivyo sasa, ubora ukoje na kwa kiasi gani na itaangalia maeneo yenye udhaifu. Kwa yale yenye ubora ni namna gani yaboreshwe zaidi na yale yenye udhaifu, ni namna gani masahihisho yafanyike ili kufanya mambo yawe mazuri zaidi. Matumaini yangu ni kwamba baada ya kazi ya tume hii, mifumo na utendaji wa vyombo hivi yataboreka," alisema.

"Yatatoka mapendekezo ambayo yatatusaidia kuboresha na kuimarisha yale ambayo yanafanyika vizuri kuyafanya yawe mazuri zaidi, kurekebisha makosa ambayo yatakuwa yamejitokeza kwa sababu wanakutana na watu wengi," aliongeza.

**MAGEREZA**

Kuhusu Magereza, Dk. Kikwete alisema mapendekezo yataamua aina ya mafunzo kwa wafungwa ili watakapomaliza kutumikia vifungo vyao wasirudie tena makosa.

Alitoa mfano kwamba nchini Uingereza, Magereza wanaita 'correction service' (huduma ya marekebisho) na visiwani Zanzibar wanaita chuo cha mafunzo kwa lengo la kuwatengeneza wafungwa kuwa raia wema wanapomaliza vifungo.

"Haya maeneo matatu makubwa wametaka nitoe maoni yangu. Nimezungumzia uzoefu wangu kwenye hayo, nimewaachia watu wa tume watapima kama niliyoyasema yana maana au hayana mashiko," alisema.

## HABARI KITAIFA



Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, wakizima moto uliokuwa unawaka kwenye nyumba namba 28 iliyopo kwenye ghorofa katika makutano ya Mtaa wa Hindi na Morogoro, jijini Dar es Salaam jana. Hakuna majeruhi.
**PICHA: JUMANNE JUMA**

# Makandarasi 500 wafutiwa usajili

**Na Rose Jacob, MWANZA**

BODI ya Usajili wa Makandarasi (CRB) imewafutia usajili zaidi ya makandarasi 500 kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kukosa sifa na wengine kuacha kazi hiyo.

Akizungumza juzi katika mkutano wa mashauriano na wadau wa sekta ya ujenzi uliofanyika jijini Mwanza, Msajili wa CRB, Mhandisi Rhoben Nkori, alisema mwaka jana bodi ilifanya tathmini kubaini baadhi ya makandarasi ambao walikuwa wamekosa sifa na kuwafutia usajili.

"Wengine wamekatisha biashara, hivyo bodi tuliamua kuwaondoa makandarasi 520 ili kubakiza wanaokidhi vigezo waweze kuendelea na kazi vilevile tulifanya usajili wa miradi 4,013 yenye thamani ya Sh. trilioni 6.1 na asilimia 50.1 ilifanywa na makandarasi wa ndani na asilimia 49.9 makandarasi wageni," alisema.

Kadhalika, alisema bodi hiyo ilikagua miradi 3,728 na kati ya hiyo miradi 2,494 ambayo ni asilimia 67 haikuwa na kasoro na miradi 1,236 sawa na asilimia 33 ilikuwa na kasoro mbalimbali, hivyo bodi ilitoa maelekezo stahiki kwa mujibu wa sheria.

Aidha, Nkori aliomba serikali kutatua adha ya utekelezaji wa kifungu cha Sheria ya Ununuzi wa Umma pamoja na kanuni zake katika eneo la dhamana za zabuni na dhamana za utekelezaji. Nkori alisema kwa mujibu wa sheria hiyo, mwajiri ndiye amepewa uwezo wa kuamua aina ya dhamana itakayotumika ambayo ni lazima itumike kwa wazabuni wote.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, alisema matumizi ya 'force account' yataendele kupungua, huku akiitaka bodi hiyo kuongeza bidii kwenye usajili, kudhibiti na kuendeleza makandarasi. Kuhusu kuweka mfumo wa kuhakikisha wataalamu wa ngazi za kati katika fani mbalimbali za ujenzi kwa kuboresha miundombinu, aliagiza kuanzishwa programu za kupokea wanafunzi wanaofanya mafunzo kwa vitendo, huku akiahidi kufanyia kazi shida zingine zilizowasilishwa kwenye mkutano huo.

# Jaji Kiongozi atupia jicho mashauri ya muda mrefu

**Na Mwandishi Wetu**

JAJI Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mustapher Siyani, amewaagiza maofisa wa mahakama, wakiwamo majaji, naibu wasajili na mahakimu kutoa kipaumbele katika kushughulikia mashauri ya muda mrefu.

Siyani alisema hayo juzi alipofanya ziara ya kikazi katika Gereza la Mahabusu Segerea, Dar es Salaam, ambako alipata fursa ya kusikiliza kero za mahabusu hao.

"Kesi iliyotangulia kuja iwe ya kwanza kupangiwa tarehe kwa ajili ya kusikilizwa na hata mashauri yaliyorudi kutoka Mahakama ya Rufani na kupata namba mpya nayo yapewe kipaumbele," alisisitiza.

Kwa upande wa mahakimu, Jaji Kiongozi aliwataka kuchapa kazi na kuhakikisha kila mmoja anamaliza kiwango cha mashauri aliyopangiwa kwa mwaka.

Pia, aliwasisitiza mahakimu wa mahakama za mwanzo kumaliza mashauri 260 na wale wa mahakama za wilaya mashauri 250. Majaji wa Mahakama Kuu kwa upande wao, wanapaswa kumaliza mashauri 220.

Akiwa katika ofisi ya Mkuu wa Gereza hilo, Jaji Kiongozi alipokea taarifa na baadaye alikagua maeneo mbalimbali ya gereza, vikiwamo vyumba wanavyolala mahabusu na jikoni wanapoandaliwa chakula.

Mahabusu wa kike na wa kiume wa gereza hilo, walimwomba Jaji Kiongozi kuwa mashauri yaliyokaa muda mrefu mahakamani yapewe kipaumbele na upepelezi ukamilishwe kwa wakati.

Katika ziara hiyo, Jaji Kiongozi Siyani aliambatana na Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Dar es Salaam, Salma Maghimbi na viongozi wa Mahakama ya Tanzania kutoka makao makuu, akiwamo Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Wilbert Chuma na Msajili wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Sharmillah Sarwatt.

# Uwekezaji viwanda PSSSF kutoa ajira 1,300

**Na Joseph Mwendapole,**
MOROGORO

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), umesema viwanda vyake vinne ambavyo umewekeza kwa ubia, vitagharimu Sh. bilioni 164 mpaka kukamilika na vitazalisha ajira 3,313 za moja kwa moja.

Maneja wa Uwekezaji wa PSSSF, Herman Goodluck, alisema hayo jana mjini hapa wakati akiwasilisha mada kuhusu uwekezaji unaofanywa na mfuko huo wakati wa mkutano wa Jukwaa la Wahariri (TEF) unaoendelea mkoani hapa.

Alivitaja viwanda hivyo kuwa ni Nguru Hills Ranch kilichoko Morogoro, Mponde Tea Tanga, Karanga International Leather Industries Limited kilichoko Moshi, Kilimanjaro na Mamba Miamba Ginger kilichoko Same, mkoani Kilimanjaro.

Goodluck alisema viwanda hivyo viko katika hatua mbalimbali za ukamilishaji wake na kwamba vitasaidia kuwapa wakulima uhakika wa masoko ya bidhaa zao hivyo kuwaondoa kwenye umaskini.

Pia alisema mfuko huo umewekeza kwenye masoko ya fedha na mitaji na kwamba uwekezaji huo umekuwa na mchango mkubwa sana kwenye kuchochea uchumi na kuongeza ajira. Alisema asilimia 60 ya uwekezaji wa mfuko huo umefanywa kwenye hati fungani ambako uwekezaji huo umeonyesha mafanikio makubwa kwa mfuko huo.

Pia alisema PSSSF imewekeza asilimia 15 kwenye ujenzi wa majengo na nyumba za kuuza na kupangisha na kwamba uwekezaji huo umekuwa ukiusaidia mfuko kwa kiwango kikubwa kukabiliana na mfumuko wa bei.

"Uwekezaji huu wa majengo na nyumba ingawa ni uwekezaji wa muda mrefu lakini unatusaidia sana kufikia malengo yetu na kutunza thamani ya mfumo pia kukabiliana na mfumuko wa bei ingawa baadhi ya hasara zake ni kwamba ukihitaji fedha ya haraka haraka huwezi kuipata, yaani huwezi ukauza sehemu ndogo ya jengo ili upate fedha za haraka," alisema.

Mfuko huo, alisema umenunua viwanja kwenye maeneo mbalimbali kama akiba na kwamba baada ya kuona mfuko unaingia gharama kubwa za kuvitunza na kuvilinda wameamua kuvipangisha kwa wafanyabiashara mbalimbali ambao wamekuwa wakifanya shughuli ambazo hazihitaji majengo ya kudumu.

Alisema wamenunua hisa kwenye taasisi mbalimbali za kifedha kama benki ya Azania ambako wana asilimia 50, Benki za CRDB, ACB, TCB na amana za kudumu (fixed deposit) asilimia 5.1.

# Mradi wa bilioni 119/- kupunguza kiu ya maji Ruangwa, Nachingwea

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa amesema serikali imeandaa mradi mkubwa wa maji wenye thamani ya Sh. bilioni 119 ambao utahudumia vijiji 34 vya wilaya ya Ruangwa na 21 vya Nachingwea mkoani Lindi.

Taarifa iliyotolewa jana na Ofisi ya Waziri Mkuu ilisema Majaliwa alisema hayo jana wakati akizungumza na wakazi wa Ruangwa waliohudhuria hafla ya kutambulisha mafanikio ya miaka miwili ya Rais Samia Suluhu Hassan madarakani, iliyofanyika kwenye ghala la Lipande, wilayani humo.

"Mradi huu utaanzia Nyangao, kuja Nanganga hadi Ruangwa kisha utaenda Chiola hadi Nachingwea. Mkandarasi ameshapatikana na mkataba umeshatiwa saini, kwa hiyo mradi utaanza wakati wowote," alisema.

"Dhamira ya Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuongeza uwezo wa upatikanaji wa maji kwenye miji yetu na vijiji vinavyozunguka miji hiyo, " alisisitiza.

Waziri Mkuu ambaye pia ni Mbunge wa Ruangwa, alitumia fursa hiyo kuelezea mafanikio yaliyopatikana kwenye sekta za elimu, afya, maji, barabara, madini na michezo.

Kuhusu elimu kwenye wilaya hiyo, alisema miundombinu imeboreshwa kwa kujenga shule mpya za sekondari na za msingi, ufundishaji umeimarika na ufaulu kuongezeka na kufikia asilimia 98. Alisema Ruangwa kuna baadhi ya kata ambazo zina shule za sekondari mbili ambapo kata ya Likunja ina sekondari za Likunja na Kitandi.

"Kata nyingine ni Narungombe kuna ambako kuna sekondari za Liugulu na Narungombe. Liugulu tumeamua iwe maalumu kwa wasichana na Narungombe iwe maalumu kwa wavulana," alisema.

Waziri Mkuu aliwapongeza walimu na wazazi kwa kuweza kudhibiti utoro wa wanafunzi na aliwapongeza wazazi kwa kusimamia nidhamu ya watoto wao na kufuatilia masomo yao.

"Tukifanya haya, tutaongeza nguvu ya walimu na azma yetu ya kutoka asilimia 98 kwenda 100 itafikiwa," alisema.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) , Abuu Jumaa, ambaye alikuwapo kwenye hafla hiyo, aliwataka wazazi wachukue tahadhari kwa watoto wao katika kipindi hiki ambacho kinakabiliwa na mmomonyoko wa maadili.

"Dunia imeharibika. Sasa hivi kuna jambo la ushoga linaendelea. Nawaomba wazazi na wananchi wa Ruangwa tukae na watoto wetu na tulisemee jambo hili. Pia Ukimwi bado upo, tatizo la dawa za kulevya lipo, yote haya lazima tuyaseme kwa vijana wetu," alisisitiza.

Naye Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alikabidhi nyaraka za ununuzi wa dawa za mkoa mzima zenye thamani ya Sh. bilioni mbili kwa Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainab Tellack, ili kuzifuatilia kwa makini kwa kila wilaya. Alisema mgawo wa mkoa mzima ulikuwa Sh. bilioni sita lakini hadi sasa mkoa umeshatumia Sh. bilioni 4.

Naibu Waziri wa Nchi (OR-TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, alisema serikali inatambua kuwa halmashauri hiyo ina upungufu wa magari ya wagonjwa na imeshalifanyia kazi suala hilo.

"Serikali imenunua magari matatu kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa. Mawili kati ya hayo ni ya kubeba wagonjwa na gari moja ni la kusafirisha chanjo. Pia watumishi wa afya tumewaleta wako 67 na walimu walioletwa hapa wako 91," alisema.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Goba Tegeta A, mkoani Dar es Salaam, wamepanda kwenye bajaji wakiwa zaidi ya 15 jana, ili dereva apate nauli ya 3,000/- na awasafirishe zaidi ya kilometa 3, kutokana na eneo hilo kutokuwepo daladala za kutosha. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# H/shauri yataja chanzo kupata hati chafu makusanyo

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI mkoani Shinyanga imetaja moja ya sababu iliyoyasabaisha Halmashauri ya Ushetu kupata hati chafu ni kuharibiwa kwa mashine zaidi 100 za ukusanyaji wa mapato (POSI) na mifumo yake.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme aliyabainisha hayo juzi akizungumza na watumishi wa halmashauri hiyo wakati wa ziara ya Kamati ya Siasa ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya kukagua utekelezaji wa ilani ya chama.

Alisema, uzembe huo hatauvumilia na amebaini watumishi hawajitumi katika utendaji wa kazi.

Mndeme alisema watumishi waliohusika kuchezea mashine hizo na mifumo yake lazima wachukuliwe hatua kali za kisheria kwani ni uzembe na kutia doa Mkoa wa Shinyanga.

Mndeme alisema wameanza uchunguzi maalumu ili kuwabaini waliosababisha halmashauri hiyo kupata hati chafu, huku akiagiza kufanyika ukaguzi wa mifumo ya kielekroniki ya ukusanyaji wa mapatao na wahusika kuwajibishwa.

"Watumishi mmefanya matumizi ya hovyo na kusababisha halmashauri kupata hati mbaya na baadhi yenu mmekuwa mkificha vocha kwa makusudi. Tutawachukulia hatua kali za kisheria wale wote watakaotajwa na kamati ya uchunguzi iliyoundwa ili tukomeshe tabia hii," alisema.

Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani, alisema kupata hati mbaya kwa halmashauri hiyo kumesababishwa na idara ya uhasibu kwa kushindwa kusimamia majukumu yao ipasavyo na kuahidi suala hilo halitaweza kutokea tena katika siku za baadaye.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Verena Ntulo alisema, kitendo cha halmashauri kupata hati mbaya kinawapa fursa ya kufanya uchunguzi ili kuwabaini watumishi wote waliohusika.

Diwani wa Nyamilangano, Robert Mihayo alisema wamesikitishwa na kitendo cha baadhi ya watumishi wasiokuwa waadilifu kuchezea mifumo ya ukusanyaji wa mapato.

Alisema kwa sasa halmashauri inataswira mbaya kwani imetia doa halmashauri nyingine za Mkoa wa shinyanga zilizofanya vema na kuomba wale wote waliosababisha wachukuliwe hatua kali za kisheria.

Hivi karibuni Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za serikali (CAG), Charles Kichere aliitaja Halmashauri ya Ushetu iliyopo wilayani Kahama Mkoani Shinyanga kuwa imepata hati chafu na kuifanya kuwa ya mwisho kati ya 184 zilizopo hapa nchini katika hesabu za serikali kwa mwaka 2022/2023.

# Bunge latoa siku 30 utatuzi soko Mabibo

**Na Mary Geofrey**

MWENYEKITI wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), Halima Mdee, ameiagiza Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kutafuta suluhu ya mgogoro wa umiliki wa ardhi katika soko la Mabibo ndani ya mwezi mmoja.

Alitoa agizo hilo wakati kamati hiyo ilipofanya ziara katika halmashauri hiyo kutembelea mradi wa soko na nyumba za Oysterbay.

Mdee aliutaka uongozi wa TAMISEMI kukaa pamoja kutafuta umiliki wa eneo la hekari tisa kutoka kwenye kiwanda hicho kinachomilikiwa kati ya Tanzania na China.

"Naomba niwape mwezi mmoja TAMISEMI mtakuwa mmeshakaa na kamati inayoshughulikia kero hii na Bunge litakuwa limeshaanza, hivyo nitaomba kukutana nanyi kujua mmefikia wapi kwa hatua zaidi," alisema Mdee.

Hata hivyo kamati hiyo ilishindwa kutembelea soko hilo kwa kile kilichodaiwa kuepuka taharuki ya wafanyabiashara hao ambao wanaamini viongozi na watumishi wa serikali wanaowatembelea wana lengo la kutaka kuwanyang'anya umiliki wake.

Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI, Dk. Charles Mahera, aliomba kamati hiyo kumpa muda kwa ajili ya kukaa na Waziri, viongozi wengine na kamati kutafuta suluhu ya kero hiyo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mkoa wa Dar es Salaam, Rehema Madenge, alisema awali wakati soko hilo likiwa linamilikiwa na halmashauri, walikuwa wanakusanya Sh. milioni 90 hadi 100 kwa mwezi lakini sasa hawapati mapato yoyote kutoka soko hilo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ubungo, Beatrice Dominic, alisema soko hilo lilikuwa likipatia halmashauri makusanyo Sh. bilioni 900 kwa mwaka, lakini kwa sasa hawana uhalali wa kuhoji wa kufuatilia makusanyo yake.

Alisema wanafuatilia ili kupata uhalali wa umiliki eneo la hekari tisa ili walikarabati soko lote na halmashauri ipate uhalali wa kukusanya mapato. Kuhusu eneo la nyumba za Oysterbay kamati hiyo ilishindwa kujadili kwa sababu kesi yake ipo mahakamani.

## HABARI KITAIFA

# Ulega anadi fursa mifugo, uvuvi ughaibuni

**Na Mwandishi Wetu,**
ROME, ITALIA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amekutana na wadau wa maendeleo kutoka taasisi na kampuni mbalimbali Italia na kujadiliana nao fursa mbalimbali ambazo wanaweza kuzitumia kuwekeza Tanzania hususan katika sekta za mifugo na uvuvi.

Ulega alikutana na wadau hao juzi jijini hapa wakati wa ziara yake ya kikazi nchini Italia.

Akizungumza na wadau hao kwa nyakati tofauti, Ulega alisema kwa sasa serikali imedhamiria kubadilisha mfumo wa uzalishaji wa sekta za mifugo na uvuvi kutoka katika kufanya shughuli za kiasili na kujiendesha kibiashara ili kuongeza uzalishaji.

Katika kuhakikisha sekta hizo mbili zinabadili mfumo wa utekelezaji kuwa wa kibiashara, alisema serikali inatekeleza Mpango wa Mabadiliko wa Sekta ya Mifugo wa Mwaka 2022/23-2026/27 na Mpango Kabambe wa Maendeleo wa Sekta ya Uvuvi wa Mwaka 2021/22-2036/37.

"Rais wetu, Dk. Samia Suluhu Hassan, amedhamiria kubadilisha mfumo wa uzalishaji wa sekta za mifugo na uvuvi kutoka katika kufanya shughuli zake kiasili na kujiendesha kibiashara, hivyo kukutana kwetu leo (juzi) ni fursa nzuri ya kujadiliana nanyi ili kuona fursa za uwekezaji katika sekta hizo mbili ambazo kufanikiwa kwake kunahitaji ushiriki wenu," alisema Ulega

Waziri Ulega alitumia fursa hiyo pia kuwaeleza wadau hao kuwa serikali ingependa kupata wawekezaji mahiri katika sekta ya mifugo hususan eneo la biashara ya nyama kwa kushirikiana na Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), kuwekeza kwenye mnyororo wa thamani katika sekta za mifugo na uvuvi hususan dagaa kutoka Ziwa Victoria.

Mkurugenzi wa Italia, anayeshughulikia nchi za Afrika, Balozi Giuseppe Mistretta, alikubali ombi la Waziri Ulega la kuiweka Tanzania kuwa miongoni mwa nchi za kipaumbele katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Aidha, Waziri Ulega alisema anatambua ushirikiano uliopo baina ya serikali na wawekezaji kutoka Italia katika kusaidia kukuza uchumi wa Tanzania huku akiwakaribisha wawekezaji wengi zaidi kufanya uwekezaji Tanzania.

Katika ziara yake hiyo, Waziri Ulega alikutana na viongozi wa taasisi ya SACE, Benki ya Uwekezaji ya Italia (CDP), Shirika la Umoja wa Mataifa la



Waziri wa Mifugo Uvuvi, Abdallah Ulega (kulia), akizungumza na Mkurugenzi wa Italia anayeshughulikia nchi za Afrika, Balozi Giuseppe Mistretta, wakati wa kikao jijini Rome, Italia juzi. Kikao hicho, kililenga kujenga uhusiano kati ya Tanzania na Italia na kuangazia fursa za uwekezaji kwa Sekta ya Mifugo na Uvuvi. **PICHA: WMU**

# DAWASA yachochea utalii pori la akiba Pande

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) imefikisha huduma ya maji katika kituo cha utalii Pori la akiba Pande hatua ambayo imelifanya eneo hilo kuwa na maji ya uhakika wakati wote, hivyo kuchochea ukuaji wa utalii.

Msimamizi wa miradi ya DAWASA Mabwepande, Mhandisi Adam Makindai, alisema jana kuwa mradi wa kuunganisha huduma katika Pori la Akiba Pande limekamilika na sasa huduma itapatikana kwa uhakika.

"Tulipokea maombi ya uhitaji wa huduma kutoka katika uongozi wa Pori la Pande na baada ya kukamilisha taratibu zote za kuunganishwa na huduma ya maji kazi hiyo imefanyika kwa haraka na sasa huduma inapatikana ambayo ilihusisha uchimbaji na ulazaji wa bomba zenye ukubwa wa inchi nne na mbili kwa umbali wa Kilomita 1.3," alisema.

Kamanda wa Uhifadhi Pori la Akiba Pande, Honest Bureta, alisema hatua ya kuunganishwa na huduma ya DAWASA itasaidia kukuza utalii na kuongeza idadi ya watalii watakaotembelea pori hilo.

"Huduma hii kwetu ni faida, utalii unaenda kukua kwa kasi, wageni wengi walishindwa kufika hapa na kupata huduma za malazi katika kambi zetu kutokana na changamoto ya huduma ya maji, jambo hili sasa limekwisha.

"Awali huduma tulikuwa tunaipata kwa kununua maji ya watoa huduma binafsi (Boza) kwa gharama kubwa na mara tatu hadi nne kwa siku hivyo huduma hii ya dawasa itapunguza sana gharama za uendeshaji," alisema Bureta.

Pori la Akiba Pande lililoko katika Wilaya ya Kinondoni ni miongoni mwa vivutio muhimu vya utalii mkoani Dar es Salaam ambalo linahusisha vivutio mbalimbali vikiwamo wanyama wadogo wadogo.

Pia lina mimea pekee inayopatikana pori la Pande pekee duniani pamoja na utalii wa ndege, bonde lililojaa uoto wa asili ndani yake na utalii wa picha.

# Madereva daladala mbaroni kukatisha safari

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MADEREVA 11 wa mabasi ya abiria maarufu kama daladala, jijini Mwanza, wamekamatwa kwa tuhuma za kukatisha safari na wanatarajiwa kufikishwa mahakamani wakati wowote kuanzia sasa.

Madereva hao wamekamatwa na Jeshi la Polisi kutokana na opereshieni ya kamatakamata iliyoanzishwa kwa lengo la kudhibiti madereva hao kukatisha safari katika njia walizopewa wakati wa kuomba leseni za uendeshaji.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, kamishna msaidizi Mwandamizi (SACP) wilbroad Mutafungwa, alisema jana kuwa madereva hao wamekuwa sugu katika uvunjaji wa sheria barabarani, hivyo jeshi hilo limeamua kukomesha vitendo hivyo.

Inadaiwa kuwa kesi nyingi za kukatisha safari zimeripotiwa katika magari yenye safari za Kisesa –Nyanshishi, Airport-Nyanshishi, Ilalila-Nyanshi na kwamba madereva hao wamekuwa wakiacha kuendelea na safari na kuwashinikiza abiria kushuka na kutafuta usafiri mbadala.

Kamanda Mutafungwa alisema baada ya kuona kesi hizo zimekuwa nyingi, wameanzisha oparesheni ambayo imefanikisha kuwanasa madereva hao 11 na kusema mchakato huo ni endelevu.

Alisema madereva hao ambao tayari wamekamatwa wanatarajia kuwafikisha mahakamani hivi karibuni ili sheria ichukue mkondo wake. Pamoja na kupelekwa mahakamani, jeshi litaendelea na kampeni hiyo mpaka litakapohakikisha tatizo hilo haliendelei tena.

"Hatutachoka kuwapeleka mahakamani haijalishi wameenda wamaliza adhabu yao wakirudi mtaani wakarudia tabia hizo tunawapeleka tena mpaka akili itawakaa sawa na kuacha vitendo hivyo," alisema SACP Mutafungwa

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Mwanza, Mrakibu Msaidizi (ASP) Sunday Ibrahim, akieleza mikakati waliyoiweka kudhibiti vitendo hivyo, alisema kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) tayari wameweka mpango wa kubandika namba za viongozi mbalimbali katika daladala zote ili abiria watakaofanyiwa vitendo hivyo watoe taarifa moja kwa moja.

Nao baadhi ya madereva wa daladala mkoani hapa, waliahidi kutokuendekeza vitendo hivyo walivyokuwa wakifanya kutoka na kuwa na abiria wachache waliosalia katika daladala zao ili kuepusha adhabu kali kutoka kwa mamlaka husika.

"Ujumbe huu utawafikia madereva wote wa mkoa wa Mwanza lengo likiwa ni kuhakikisha watu tunaowahudumia hawakumbani na adha kama hizi sambamba na kufuata sheria zilizowekwa," alisema Mrajifu Manyani, Mwenyekiti wa Madereva wa Daladala Mkoa wa Mwanza.

Vitarino Ngonyani, mwakilishi wa LATRA, alisema kwa mujibu wa sheria na kanuni za mamlaka hiyo, kitendo cha dereva kutokufika mwisho wa safari ni kinyuma cha Sheria ya Kanuni namba 24 b (i) na faini yake si chini ya Sh.100,000

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ukarabati wa viwanja Bara ufuate mwongozo wa CAF

**ZIKIWA** zimepita siku chache tangu mechi kati ya Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), dhidi ya Uganda (The Cranes), kusimama kwa zaidi ya dakika 30 kutokana na changamoto ya taa kuzimika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Serikali imetangaza itanunua jenereta mpya mbili ili kukabiliana na tatizo hilo siku za usoni.

Mechi hiyo iliyomalizika na Taifa Stars kufungwa bao 1-0 na The Cranes, ilinusurika kuvunjika kutokana na umeme kuchelewa kurejea kwa wakati na ilibainika uwanja huo unatumia jenereta moja tu, tofauti na hali ilivyo katika viwanja vingine vya nchi zilizoendelea.

Wamiliki wa viwanja hutumia jenereta ili kuonyesha mechi kwa sababu ya kutokuwa na imani na umeme wa kawaida kwenye mchezo huo muhimu ambao hushuhudiwa mubashara na idadi kubwa ya mashabiki.

Ikumbukwe Uwanja wa Benjamin Mkapa si tu unatumiwa na timu za Simba, Yanga, Taifa Stars na klabu nyingine zinapokuwa na majukumu ya kimataifa, pia imeshapokea klabu kutoka Burundi, Sudan Kusini ambazo zimekosa vibali vya kutumia viwanja vya nyumbani kwao kutokana na sababu mbalimbali.

Baada ya janga hilo kutokea, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dkt. Pindi Chana, mwishoni mwa wiki hii ametangaza serikali imeshaanza mchakato wa kununua jenereta mpya mbili ili kumaliza tatizo hilo lililojitokeza kwenye uwanja huo mkubwa na wa kisasa nchini.

Tatizo la umeme lilitokea tena mbele ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika mchezo huo wa kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2023). Hakika lilikuwa jambo la kuhuzunisha,pia limesaidia kuwafumbua macho wahusika.

Kabla ya tukio hilo, tayari Shirikisho la Soka Afrika (CAF), lilishatoa maelekezo kuhusiana na marekebisho muhimu yanayotakiwa kufanyika kwenye uwanja huo ili uendelee kupata baraka ya michezo ya kimataifa kufanyika.

Katika macho ya kawaida, unaweza kusema marekebisho hayo yananza kufanyika, zaidi ya kushuhudia Simba na Yanga zikihamisha michezo yake ya Ligi Kuu Tanzania Bara na kuupunguzia matumizi uwanja huo hasa kwenye eneo la kuchezea ambalo 'vipara' vilianza kuonekana kwa nyasi zake kushindwa kuota vizuri.

Lakini, maofisa wa CAF walitoa maelekezo kwa maandishi, hivyo tunawaomba wahusika kuhakikisha wanakamilisha maboresho yote katika kiwango cha juu na kuufanya uwanja huo unaopendwa kurejea katika hadhi yake.

Tunawakumbusha wasimamizi wa uwanja kuhakikisha wanalifanyia kwa vitendo suala la kupata umeme wa uhakika kwenye uwanja huo ili mashindano makubwa ya Super Cup ambayo yanatarajiwa kufanyika baadaye mwaka huu na Simba ikipata tiketi ya kushiriki yachezwe hapo na si kuhamishiwa kwingine.


Mbali na suala la umeme, Waziri Chana amesema pia serikali itaanza mchakato wa kufanya matengenezo katika viwanja vingine vya soka vilivyoko mikoani (Dodoma, Tanga, Mwanza na Arusha), ili miundombinu hiyo irejee kwenye ubora unaotambulika.

Ni vyema maandalizi ya ukarabati huo yakaanza sasa wakati msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2022/2023 unaelekea ukingoni, kila timu imeshacheza mechi 24 na zimebakia michezo sita ili kumaliza msimu.

Viwanja hivyo vikifanyiwa ukarabati mapema, tunaamini msimu ujao vitasaidia kutumika katika michezo mbalimbali na kuupa 'ahueni' Uwanja wa Benjamin Mkapa ambao umekuwa ukitumika mfululizo.

Umefika wakati Tanzania tukajifunza kutoka kwa wenzetu ambao uwanja wao mkubwa hutumika kwa michezo mikubwa ya Timu za Taifa au klabu zake zinapokabiliwa na mechi kubwa na si kila mchezo kufanyika hapo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Utafutwe mwarobaini, Stars 'kulala' nyumbani

**ILIKUWA** kama ndoto Jumanne iliyopita pale mwamuzi, Ahmad Heeralall, kutoka Mauritius alipopuliza kipenga kuashiria kumalizika kwa mechi ya raundi ya nne ya kusaka tiketi ya kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON 2023), Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), ikiwa imepoteza kwa bao 1-0 dhidi ya Uganda (The Cranes).

Si mashabiki waliokuwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, waliokuwa wakiangalia kupitia televisheni au waliokuwa wakisikiliza kwenye redio walioamini Taifa Stars imechapwa bao 1-0 kwa sababu kadhaa.

Kwanza kabisa ni bao lililokuja ghafla sana, na likafungwa mwishoni mwa mchezo, dakika ya 90. Halikuwa ni shambulizi lililotengenezwa kwa muda mrefu, hivyo kulionekana hakuna hatari yoyote.

Wakati Stars ikisaka kwa nguvu bao kwani mpaka wakati huo mambo yalikuwa suluhu, huku mashabiki uwanjani wakishinikiza kwa kushangilia, mpira uliokolewa na katikati ya uwanja ulimkuta Farouk Miya ambaye alipiga pasi moja ndefu, lakini iliyokatiza eneo hatari na kuwaacha mabeki na viungo wakipotezana na kumkuta, Rodgers Mato, aliyeukwamisha wavuni.

Uwanja ukawa kimya, na kila mtu hakuamini kilichotokea. Kingine ambacho mashabiki wa Kibongo walikuwa na furaha ya ushindi walioupata Misri siku chache zilizopita.

Kwenye Uwanja wa Suez Canal, Ismailia nchini Misri, Stars ilishinda bao 1-0 dhidi ya Uganda ambayo iliutumia uwanja huo kutokana na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF) kuvifungia viwanja vyao kutokana na kukosa ubora unaohitajika.

Ushindi huo wa bao la Simon Msuva, wengi waliweka uhakika kama ugenini Tanzania imeshinda basi nyumbani si tu kama itapata ushindi lakini wa mabao mengi pia. Haikuwa hivyo. Mechi tangu mwanzo ilionekana ngumu kuliko hata ilivyokuwa ile ya kwanza.

Pamoja na ugumu huo lakini bado haikuonekana inakaribia kufungwa. Wengi baada ya Stars kupoteza walianza kuongea maneno mengi ya kuiponda timu. Wapondani ni wale wale ambao waliisifia iliposhinda nchini Misri.

Mashabiki wengi na hata wachambuzi wamekuwa wakiikosoa Stars inapopoteza bila kuangalia takwimu kwanza zinasemaje.

Takwimu, wakati mwingine zinasaidia kuangalia timu ifanye nini. Kama takwimu zinaonyesha timu inashinda sana nyumbani na kupoteza ugenini huwa inawasaidia makocha kujua nini wafanye ili kushinda ugenini.

Tanzania haina timu mbaya, au wachezaji wana matatizo la hasha, ndiyo maana huwa inafanya vyema sana inapocheza nje ya ardhi ya nyumbani. Tatizo la Stars ni pale inapokuja kucheza kwenye ardhi yake ya nyumbani. Na wala hili si la mwaka huu au mwaka jana. Lilianza mwaka 2007, wakati Stars ikiihitaji ushindi ili kufuzu fainali za AFCON mwaka 2008 na ilikuwa ikicheza dhidi ya Msumbuji. Kilichotokea kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa wakati huo ukiitwa Uwanja wa Taifa, Stars ilifungwa bao 1-0 lililowekwa wavuni na straika hatari wakati huo Tico Tico. Kipigo hicho kilitokea wakati Stars ikiwa imetoa suluhu ugenini, hivyo kila shabiki alijua Stars itashinda.

Mwaka 2021 kwenye mechi za kusaka tiketi ya kwenda kucheza Fainali za Kombe la Dunia nchini Qatar mwaka jana, Stars iliichapwa bao 1-0 na Benin nyumbani, lakini ilipoenda ugenini ikashinda bao 1-0.

Kwenye michuano hiyo, ilitoa sare ya bao 1-1 nchini Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo dhidi ya timu yao ya taifa, lakini ikachapika nyumbani magoli 3-0. Hiyo ni mifano michache tu. Sasa cha kujiuliza. Ni kwa nini Stars haifanyi vyema ikicheza nchini?

Wachezaji wanapata presha gani wakicheza mbele ya mashabiki wao? Je huwa wanacheza vyema ugenini kwa sababu wanakuwa hawana presha ya mashabiki wa nje? Kwa nini timu za Simba na Yanga ambazo zina baadhi ya wachezaji walio Taifa Stars wanautumia vizuri Uwanja wa Benjamin Mkapa na kuufanya machinjio wakati Stars inakuwa kinyume. Hapa kuna kitu cha kujadili na kukifanyia kazi ili tatizo lijulikane kwa ajili ya mustakabali wa mechi zijazo.

Hata hivyo, tusiache, tuendelee kuiunga mkono Taifa Stars katika mechi zinazofuata.

## HABARI KITAIFA




Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule akizungumza wakati akifungua kikao kazi cha wadau wa elimu jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mfumo mpya upimaji wa utendaji kazi kuwabana maofisa utumishi

**Na James Mwanamyoto,**
DODOMA

MFUMO mpya wa kupima utendaji kazi wa watumishi wa umma utatumika kubaini mikoa na halmashauri ambazo zinaongoza kukwepa kutoa ufafanuzi wa masuala ya kiutumishi, imeelezwa.

Halmashauri hizo badala ya kutatua masuala hayo, huwasilisha barua kwa Katibu Mkuu UTUMISHI kuomba ufafanuzi wa masuala ambayo mikoa na halmashauri zina uwezo wa kutoa ufafanuzi kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyopo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Jenista Mhagama alisema hayo juzi jijini hapa wakati akizungumza na wanasheria na maofisa utumishi kutoka katika sekretarieti za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kabla ya kufungua kikao kazi cha maofisa hao kilicholenga kuzitafutia ufumbuzi changamoto wanazokabiliana nazo katika utekelezaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma na kanuni zake.

Mhagama alisema mfumo huo utawaweka kwenye kundi la kutowajibika watumishi wote watakaosababisha mikoa na halmashauri zao kukwepa kutoa ufafanuzi wa masuala ya kiutumishi kwa kusingizia kuwa masuala hayo yanapaswa kutolewa ufanuzi na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Waziri Mhagama alihoji kwa nini mwajiri amemwandikia barua Katibu Mkuu - Utumishi kuomba ufafanuzi wa jambo wakati mwajiri huyo anaye ofisa utumishi ambaye akishirikiana vizuri na mwanasheria, kwa kutumia nyaraka zilizopo, wana uwezo mkubwa wa kulitolea uamuzi jambo husika.

"Maofisa utumishi na wanasheria mnapaswa kushirikiana katika kutoa ufafanuzi na kufanya uamuzi wa masuala ya kiutumishi kwa mujibu wa kanuni, sheria, taratibu na miongozo ya kiutumishi badala ya kukwepa jukumu hilo," alisema.

Mkurugenzi wa Huduma za Sheria, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Hilda Kabissa, alisema kikao kazi hicho kimelenga kuibua na kuzitafutia ufumbuzi changamoto za utekelezaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma na kanuni zake hususani wakati wa kushughulikia masuala ya kinidhamu.

Mmoja wa washiriki wa kikao kazi hicho, ambaye ni Ofisa Utumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, Alice Lunyata, alisema amejipanga kutekeleza maelekezo ya Waziri ya kupunguza kuwasilisha maombi Utumishi ya kupatiwa ufafanuzi wa masuala ya kiutumishi kwa kuwaelekeza, kuwapatia ufafanuzi na kuwaelimisha watumishi wa umma kuhusiana na masuala yao kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya utumishi wa umma.

Mshiriki mwingine, Ofisa Sheria wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba, Zuberi Sarahani, alsiema yeye pamoja na wanasheria wenzake watashirikiana na maofisa utumishi katika kutoa tafsiri sahihi ya sheria, kanuni, taratibu na miongozo ili kupunguza idadi ya barua za kuomba ufafanuzi.

Naye Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Tamko Ally, alisema baada ya kupokea maelekezo ya Waziri, watashirikiana na wanasheria kusoma nyaraka na kuchambua hoja zilizowasilishwa katika taasisi zao.

Kikao kazi hicho kilichoandaliwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kilihudhuriwa na maafisa utumishi na wanasheria kutoa sekretarieti za mikoa 16 na halmashauri 84.

# Botswana waja kujifunza kuhusu TEHAMA

**Na Frank Monyo**

WATAALAM kutoka Ofisi ya Kumbukumbu na Nyaraka Botswana wametembelea Ofisi za Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) kwa lengo la kujifunza taasisi hiyo inavyotumia mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Serikali wa Botswana, Gopolang Maakwe, alisema jana kuwa nchi yake iko katika mchakato wa kutengeneza mfumo wake wa ofisi mtandao kwa ajili ya kurahisisha utoaji huduma kwa wananchi.

Akizungumza alipotembelea Ofisi za OSHA na kufanya kikao na menejimenti, alisema wameona ni muhimu kujifunza kwa nchi ambazo zimepiga hatua katika matumizi ya mifumo hiyo.

"Tumekuja hapa kujifunza namna ambavyo Tanzania imefanikiwa kujenga na kutumia mfumo wa ofisi mtandao katika taasisi zake zaidi ya 200. Tuliposikia Tanzania wamefanikiwa katika eneo hili, tukaona ni vyema akawa mshirika wetu katika azma yetu ya kuhakikisha serikali nzima ya Botswana inaingia katika matumizi ya ofisi mtandao kuanzia mwaka 2024/25," alisema Maakwe.

"Katika ziara hii tumefurahi kusikia kwamba mfumo unaotumika Tanzania umeandaliwa kwa kutumia wataalam wa ndani, hivyo hata uangalizi na matengenezo yake hayatakuwa na gharama kubwa kwani mara nyingi uundaji wa mifumo ya TEHEMA umekuwa ukitegemea watoa huduma wa nje ya serikali jambo ambalo limekuwa likiongeza gharama za uendeshaji," aliongeza.

Aliishukuru OSHA na serikali ya Tanzania kwa ujumla kwa ukarimu na kuahidi kwamba wataendelea kuja kujifunza zaidi hadi hapo watakapokamilisha mfumo wa nchi yao.

Kaimu Mkurugenzi wa Usalama wa OSHA, Dk. Jerome Materu, alimshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuiwezesha OSHA kutumia mfumo wa ofisi mtandao na mifumo mingine ya serikali ambayo imesaidia kuongeza ufanisi katika utendaji wa OSHA.

"Mfumo wa ofisi mtandao pamoja na mifumo mingine iliyoandaliwa na serikali yetu imesaidia sana kupunguza urasimu na kutuongezea kasi ya kuwahudumia Watanzania. Sisi OSHA tunao mfumo wetu wa ndani wa usimamizi wa taarifa za maeneo ya kazi nchini ujulikanao kama WIMS ambao tunautumia sambamba na mfumo wa ofisi mtandao na mifumo mingine ya serikali katika kuwahudumia wadau wetu," alisema.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, kabla ya kuanza kutumia mifumo hiyo kulikuwa na changamoto katika upatikanaji wa huduma za OSHA. Cheti cha usajili wa eneo la kazi kilikuwa kinapatikana baada ya siku saba huku cheti cha kukidhi viwango vya usalama na afya kikiandaliwa kwa mwezi mzima.

# Vifaa kielektroniki vitakavyoingizwa nchini kukaguliwa

**Na Mary Geofrey**

KUTOKANA na kuwapo kwa ongezeko la taka zitokanazo na vifaa vya kielektroniki nchini, serikali imetangaza kuanzia Mei 23, mwaka huu vifaa vyote vya aina hiyo vinavyoagizwa kutoka nje ya nchi vitaanza kukaguliwa.

Hatua hiyo imefuatia maazimio ya Mkutano wa Taasisi za Mawasiliano Afrika Mashariki (EACO), nchi wanachama kuchukua hatua madhubuti za kudhibiti uingizaji wa vifaa vya kielektroniki vilivyoisha muda wake na ongezeko la taka hizo.

Takwimu za mwaka 2019, zinaonyesha nchini kuna tani 19,000 za taka zitokanazo na vifaa vya kielektroniki ambazo nyingi zinakuja kama msaada wa vifaa vya mawasiliano nchini kumbe vimeisha muda wake na zinazotokana na vifaa hivyo kuisha muda wa matumizi. Hatua hiyo ya serikali, ilitangazwa jana na Kaimu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA), John Daffa, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Aidha, aliwataka watengenezaji na waingizaji wa vifaa hivyo, kulipa ada ya usimamizi wa taka za kielektroniki kwa kila kifaa kinachoingizwa kama gharama za usimamizi wa vifaa hivyo vinapofika mwisho wa matumizi.

Alisema kuwa kanuni za ubora wa vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki na usimamizi wa taka za kielektroniki za mwaka 2020 zinaelekeza kuhakikisha vifaa vyote vinavyoingia nchini havijafika mwisho wa matumizi.

Daffa, alisema kanuni hizo zinataka kuhakikisha kuwa vifaa vyote vilivyofika mwisho wa matumizi vinapelekwa kwa watoa huduma wenye leseni za kukusanya, kukarabati au kuendesha mitambo ya kuchakata vifaa vya mawasiliano pale vinapofika mwisho wa matumizi.

Daffa alisema TCRA ina jukumu la kusajili taarifa za vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki ambavyo vimeingizwa au kutengenezwa nchini pamoja na kuweka makubaliano na watoa huduma waliopewa leseni kwa ajili ya kukusanya na kuendesha mitambo ya kuchakatwa taka za kielektroniki.

Alisema baada ya maombi yao kupokelewa, uchambuzi na tathmini kuhusiana na vifaa vitakavyoingizwa pamoja na ada ya usimamizi wa taka za kielektroniki itafanyika ili kuruhusu hatua za utekelezaji.

Uingizaji wa vifaa vya mawasiliano nchini, alisema unahitaji leseni tofauti yaani Importation License na vifaa vyote vitakavyoingizwa nchini vinatakiwa kuhakikiwa ili kutathmini ulinganifu na mwingiliano wakati wa matumizi.

Hata hivyo, alisema kuwa mtumiaji wa vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki hatahusika katika gharama hizo na kwamba hakutakuwa na ongezeko la gharama za ununuzi wa vifaa hivyo hapa nchini.

Alisisitiza kuwa TCRA itashirikiana na Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), katika usimamizi wa taka

# Watalii wamiminika Hifadhi ya Serengeti

**Na Mary Mosha,** HAI

WATALII 298 kutoka India, Israel na Ethiopia, wametua nchini jana, kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), kwa ajili ya kufanya utalii wa siku tisa katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA).

Wageni hao walipokewa na Mkurugenzi wa Kampuni ya Uendelezaji na Uendeshaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KADCO), Christine Mwakatobe.

Akizungumzia ugeni huo, Mwakatobe alisema watalii hao waliingia nchini kwa kutumia ndege aina ya Boeing 757 yenye abiria 65 kutoka India, Boeing 738 Max, yenye abiria 158 ikitokea moja kwa moja Israel na Boeing 787-800 iliyokuwa na abiria 75 ikitokea Addis Ababa, Ethiopia ikiwa imebeba raia wa Marekani.

"Kimsingi, ujio wa ndege hizi ni matokeo ya utangazaji wa vivutio vyetu vya utalii nje ya nchi, kupitia filamu ya The Royal Tour.

"Kwa sasa kumekuwa na mafuriko ya watalii, ongezeko la wawekezaji pamoja na wafanyabiashara. Tanzania tumekuwa wasambazaji wakubwa wa mboga na matunda katika nchi mbalimbali duniani, ndiyo maana unawaona wanavyovutiwa kuja kuona hifadhi zetu."

Baadhi yao watalii hao, akiwamo Karoly Nikoliche (59), alisema kuja kwao Tanzania kunatokana na utajiri na urithi wa wanyamapori adhimu waliko katika eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti.

"Tumekuja nchini Tanzania kwa ajili ya kufanya ziara ya siku tisa katika mbuga za wanyama, hii ni mara yangu ya kwanza kufika nchi hii, nikiongozwa na bibi na babu yangu," alisema Yael Yanger (12).

Raia wa Marekani, Gag Seav (19), alisema kuwa matembezi hayo yatawasaidia kujionea yale waliyojifunza kwenye vitabu, hasa kuhusu wanyama na tabia zao.

Wakati huo huo, jana Tanzania ilisafirisha kwa Shirika la Ndege Qatar Airways, nyama tani 17 na maua na mboga tani mbili kwenda Mashariki ya Kati (Falme za Kiarabu) na Ulaya.

Alisema walipokuwa wanafunga mwaka 2021/22 kulikuwa na abiria zaidi ya 620, hadi kufikia Februari 2023, walifika abiria 659.



Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Joseph Mkumbi (kushoto), akizungumza na wananchi wa kata ya Kwafungo, wilayani humo hivi karibuni, wakati akitoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa na programu mpya ya TAKUKURU Rafiki. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wataka muswada mabadiliko Sheria ya Ndoa 1971 kuwasilishwa bungeni

**Na Elizabeth Zaya**

MASHIRIKA ya kutetea haki za wasichana Tanzania, yameitaka serikali kuwasilisha muswada wa mabadiliko ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 katika Bunge la bajeti lijalo.

Wamesema wanataka katika muswada wa mabadiliko hayo utambue kuwa umri wa chini wa msichana kuolewa au mvulana kuoa ni miaka 18.

Wakitoa tamko hilo juzi Dar es Salaam, wadau wa mashirika hayo walisema ni miaka minne tangu Mahakama ya Rufani ilipotoa amri kwa serikali kufanyia marekebisho sheria hiyo, lakini mpaka sasa hakuna hatua iliyofanyika.

Akizungumza kwa niaba ya mashirika hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Msichana Initiative, Rebeca Gyumi, alisema vifungu ambavyo vilitolewa amri na Mahakama ya Rufani kufanyiwa marekebisho ni vya 13 na 17 ambavyo vinaruhusu mtoto wa miaka 14 kuolewa kwa kibali cha mahakama na 15 kwa ridhaa ya wazazi.

"Tunataka serikali kuwasilisha muswada na ambao unazingatia ushiriki wa wadau wa maoni yaliyotolewa ili kuwa na sheria ambayo haitakuwa na vifungu vinavyoendeleza ndoa za ututoni nchini na kubariki ukatili kwa watoto," alisema Gyumi.

"Kwa miaka minne serikali sasa kupitia muhimili wa Bunge na Wizara ya Katiba na Sheria, imeshindwa kutekeleza kwa wakati na kuchukua hatua stahiki za haraka kufanya marekebisho ya sheria hiyo ya ndoa, licha ya Mahakama ya Rufani kutoa amri ya kufanya hivyo kupitia kesi ya Rebeca Gyumi."

Aliwakumbusha wabunge kuwa wajibu wa kuwalinda watoto na ndoa za ututoni bila kujali kama wanasoma au hawasomi ni la kila mtu kwa kuwa bado ni watoto.

"Hakuna maendeleo tutakayoyafikia kama nchi bila kutokomeza ndoa za ututoni maana zinaathiri wasichana wengi na tabaka la chini ambalo ni maskini, kuwa na sheria inayohamasisha ndoa za ututoni ni kuendeleza mzunguko wa umaskini katika taifa na kuwanyima wasichana hasa wanaotoka familia maskini au vijijini," alisema Gyumi.

# Wakulima wadogo kujengewa uwezo, uhakika wa soko

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Korea (KOICA), wamezindua mradi wa kuwasaidia wakulima wadogo katika wilaya tatu za Mkoa wa Kigoma kulima kilimo biashara na kuwapa uhakika wa soko.

Mradi huo uliopewa jina la Kilimo Tija Kigoma (KiTiKi) utatekelezwa kwenye Wilaya ya Kasulu, Kibondo na Kakonko huku KOICA ikitoa Dola za Marekani milioni sita kutekeleza mradi huo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mradi huo juzi, Mwakilishi Mkazi na Mkurugenzi wa WFP nchini Tanzania, Sarah Gordon-Gibson, alisema mradi huo una lenga kuwainua wakulima wadogo na kukuza uchumi wao pia kuwezesha wakimbizi kwenye kambi za Nduta na Nyarugusu kupata mahitaji sahihi ya Chakula.

"Mradi huu utawapa fursa wakulima wadogo wa mazao kama maharage, mihogo na mahindi kulima kisasa na kuwa na soko la uhakika, mazao yatakayonunuliwa yatatumika kwenye kambi za wakimbizi za Nduta na Nyarugusu," alisema Sarah.

Aidha, Mkurugenzi wa KOICA nchini Tanzania, Manshik Shin alisema ushirikiano kwenye mradi huo ni muendelezo wao wa ushirikiano na WFP.

"Zaidi ya wakulima 20,000 katika wilaya hizi tatu wataenda kunufaika na mradi huu, lakini pia wakimbizi zaidi ya 200,000 wataenda kunufaika kwa kupata chakula cha uhakika," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Wizara ya Kilimo, Monica Kwanara, alisema serikali inawapongeza WFP kwa kuzindua mradi huo ambao utawasaidia wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao ya kimkakati yanayotumiwa na shirika hilo kwa ajili ya wakimbizi.

"Wizara inasimamia ajenda ya kilimo ya 10/30 ambapo kilimo kitakuwa kinachangia asilimia 10 kwenye pato la taifa ifikapo mwaka 2030, lakini pia mradi huu unaenda kuongeza tija kwa wakulima wa Mkoa wa Kigoma, kuongeza uzalishaji huku wakiwa na uhakika wa soko, tunawapongeza sana WFP na KOICA," alisema Kwanara.

Uzinduzi huo ulihudhuriwa na Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Thobias Andengenye ambaye aliwataka wananchi wa mkoa huo kutumia fursa ya uwepo wa mradi huo kujiongezea kipato kwa kuongeza uzalishaji zaidi.

Mradi huo utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2023-2027.



## HABARI DODOMA

# Dk. Yonazi akunwa utekelezaji miradi ya ujenzi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

KATIBU Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Dk. Jim Yonazi amesemaameridhishwa na maendeleo ya miradi ya ujenzi inayosimamiwa na ofisi hiyo.

Amesema itakapokamilika itawawezesha watumishi kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

Dk. Yonazi aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na wakuu wa idara na wakurugenzi wa ofisi hiyo kwenye ziara ya kukagua ujenzi wa maeneo yenye miradi iliyopo chini ya ofisi hiyo.

Alisema kuwa uamuzi wa serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, wa kutekeleza miradi hiyo mikubwa ni kuhakikisha shughuli za serikali zinafanyika katika mazingira yenye ubora na kuhudumia wananchi kwa weledi.

Dk. Yonazi pia alihimiza makandarasi kuhakikisha wanapata vifaa kwa wakati ili ujenzi huo ukamilike ndani ya muda uliopangwa pamoja na wasimamizi kusimamia kikamilifu majengo hayo yanakuwa na ubora unaotakiwa.

Aidha, aliwataka watumishi wa ofisi hiyo pia kuongeza ubunifu wa utendaji kazi hatua ambayo itasaidia kuhamasisha kazi kufanyika kwa mwamko na ubora zaidi .

Mkadiriaji Ujenzi kutoka Chuo Kikuu cha Ardhi, Mhandisi Saudeni Anania, aliishukuru serikali kwa kuendelea kushirikiana nao, huku akisema kuwa wanakabiliwa na tatizo la vifaa vya umaliaziaji ujenzi.

# TANESCO waagizwa kuanzisha dawati la jinsia

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Nishati, Stephen Byabato amewaagiza viongozi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuhakikisha wanaunda dawati na kitengo maalumu kitakachokuwa kinasikiliza na kushughulika kero za kijinsia kwenye shirika hilo.

Alitoa agizo hilo jana kwenye uzinduzi wa programu ya mpango wa jinsia wa miaka minne 2023-2027 wa kuhamasisha masuala ya kijinsia kwenye shirika hilo wakati wa utekelezaji wa mradi wa umeme wa Tanzania hadi Zambia uliofanyika jijini hapa.

Naibu Waziri huyo aliwataka TANESCO kuhakikisha wanaunda dawati na kitengo cha kijinsia kitakachoshughulika na mambo yote kero za kijnsia kwenye eneo lao la kazi .

Alibanisha kuwa mpango huo wa kijinsia ni sehemu ya kipengele kwenye utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme mkubwa kuanzia Tanzania hadi Zambia ujulikanao kama Tanzania -Zambia Transmission Interconector Project (TAZA).

Hata hivyo, alitaka watu watakaosimamia dawati na kitengo hicho kuwa waadilifu ili kutunza siri za watumishi watakaofika hapo kutoa malalamiko yao ya kijinsia.

Alisema, lengo la uwepo wa kitengo hicho itasaidia kupunguza malalamiko ya kijinsia kwa upande wa kike na kiume kwenye eneo hilo la shirika na kuleta masuala ya usawa katika ngazi za uongozi na sehemu ya maamuzi ya shirika hilo.

Aidha, alisema programu ya kijinsia inatekelezwa kupitia mradi huo wa nia kubwa ya umeme kuanzia Tanzania mkoani Iringa hadi nchini Zambia na inatarajiwa kugharimu Dola za Marekani milioni 600.

Alisema, kutakuwepo kwa nafasi za mafunzo ya ukuzaji wa taaluma kwa wafanyakazi wanawake waliopo kazini ili kuwajengea uwezo wa kuelekea kwenye ajira kamili.

Mkurungenzi Mkuu wa Shirika hilo, Maharage Chande alisema TANESCO wanatekeleza mradi wa ujenzi wa upanuzi wa njia ya kusafirisha umeme wa kilovoti 400 kutoka katika kituo cha kupokea, kupoza na kusafirisha umeme cha Tagamenda Iringa kwenda kwenye nchi zilizopo kusini mwa Tanzania.

Chande alisema umeme huo utapitia Kisanda Iringa, Iganjo mkoani Mbeya na Nkangamo Tuduma mkoani Songwe, kwamba unafadhiliwa na Benki ya Dunia (WB), IDA kwa mkopo wa Dola za Marekani milioni 455.

Mkopo mwingine ni kutoka Mfuko wa Maendeleo wa Ufaransa (AFD) wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 30 pamoja na Tanzania iliyotoa mkopo wa Dola za Marekani milioni 10.

Aidha, alisema kituo cha Tagamenda pia ni kitovu cha kusafirisha umeme mkubwa wa kilovoti 220 kwenda kwenye mikoa 18 nchini na kimeunganishwa na kituo cha umeme cha Zuzu mkoani Dodoma.

Alisema, sababu ya kuunganishwa na kituo hicho cha Zuzu ili kusafirisha umeme mkubwa kwenda nchi za Kenya, Uganda na Ethiopia.



Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Dk. Jim Yonazi (kulia), akikagua maendeleo ya ujenzi wa jengo la ofisi ya mpiga chapa mkuu wa serikali, eneo la Kisasa, Jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Halmashauri zaonywa urasimu fedha za asilimia 10

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, amezionya halmashauri za wilaya na manispaa nchini kuacha urasimu wa kutoa fedha zilizotolewa kwa vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Alitoa maagizo hayo juzi katika ziara ya kukagua miradi inayotekelezwa inayotokana na asilimia 10 za mapato ya halmashauri wakati akizungumza na viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi mkoani hapa.

Hatua ya Katambi kutoa maagizo hayo ilifuatia baada ya Mwenyekiti wa kikundi cha Vijana Chapa Kazi, Mwanahamisi Omari, kulalamikia kucheleweshewa kupatiwa fedha za kulipia tripu 50 za mchanga wanaotumia kufyatua matofali baada ya halmashauri hiyo kuwapa mkopo wa Sh. milioni 25.

"Mheshimiwa Naibu Waziri tunatatizo kubwa ambalo inatukwamisha na kushindwa kuendelea na ufyatuaji wa matofali fedha yetu tuliyopewa awali imekwisha sasa ni siku ya tatu kila tukienda pale halmashauri tunapigwa danadana hasa pale ofisi ya maendeleo ya jamii mara tunaambiwa hela hizo zitatolewa mpaka mhandisi aje kwenye mradi kuhakikisha kama mchanga huo upo, mara tumsubiri mkurugenzi jambo ambalo linatuchelewesha," alisema Omari.

Katambi baada ya kupokea malalamiko hayo akazitaka halmashauri zote kuacha kufanya urasimu huo akisema fedha hizo zinatolewa na halmashauri kwa lengo la kuyasaidia makundi hayo na unapojitokeza urasimu huo unarudisha nyuma maendeleo ya walengwa hao.

Aidha, Katambi aliagiza taasisi zote za serikali zinapotekeleza miradi ikiwemo ya maji na ujenzi wa madarasa na miundombinu mbalimbali itoe kazi hizo kwa kununua matofali, vifaa vya chuma na vifaa vingine kutoka katika vikundi hivyo ili vikuze mitaji yao.

Katambi alisema, taasisi hizo zinapofanya sherehe zao hasa katika mikoa ambayo ina vyuo vya ufundi ziwe zinakwenda kununua keki, upambaji na sare zinazotengezwa na wanafunzi wa vyuo hivyo ikiwamo za Chama Cha Mapinduzi (CCM) pamoja na bendera ya taifa ili kuviinua kiuchumi badala ya kwenda kuagiza nje.

Aidha, aliwataka walengwa hao kuondoa dhana ya kuwa wajasiriamali badala yake wawe wafanyabiashara wa kati na hata kufikia hatua ya kufungua kampuni zao kubwa.

Katambi pia aliziagiza halmashauri kuviongezea vikundi vinavyofanya vizuri kurejesha mikopo inayokopeshwa akikitolea mfano kikundi cha vijana cha St.Vidicon Manyoni Computer Workshop ambacho kilianzishwa Julai 2020 chini ya umoja wa mafundi wenye ujuzi wa fani mbalimbali waliokubaliana kufanya kazi kwa kushirikiana.

Alisema, wanafunzi wanaopata fursa ya mafunzo ya miezi mitatu yanayowezeshwa bure na Ofisi ya Waziri Mkuu wanapomaliza mafunzo yao halmashauri iwe inawapa mikopo kwa ajili ya kufungua viwanda vidogo badala ya kukaa mtaani na ujuzi wao.





## Viongozi mabaraza wahimizwa kutoa maoni kuhusu udhalilishaji wanawake, watoto

**Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imetiliana saini mkataba wa usimamizi wa eneo la Hifadhi ya Kisiwa cha Mnemba na Kampuni ya Beyond ambao utasaidia kuongeza makusanyo.

Akizungumza jana baada ya utiaji wa saini wa makubaliano hayo Waziri wa wizara hiyo, Masoud Suleiman Makame, alisema makubaliano hayo yataongeza idadi ya makusanyo ya idara ya uhifadhi wa bahari kutoka Sh.bilioni 1.2 hadi Sh.bilioni tatu kwa mwaka 2023/2024.

Alisema kwamba mapato hayo yataongezeka kama serikali itaridhia upitiaji upya wa tozo kutokana na shughuli mbalimbali na michezo ya watalii yanayofanyika baharini.

Aidha, alisema tozo ambazo zinatolewa kwa sasa ni ndogo ikilinganishwa na tozo za nchi nyingine kwenye ukanda wa magharibi mwa Bahari ya Hindi.

"Ongezeko hili la mapato litakalotokana na mkataba huu lina faida kubwa kwa jamii iliyo ndani ya Hifadhi ya Mnemba (MIMCA), kwa sababu asilimia 30 ya mapato yatakayokusanywa inarudi kwao kutatua changamoto zao mbali mbali za kimaendeleo na za uhifadhi wa rasilimali Bahari," alisema Makame.

Hata hivyo alisema mapato hayo yataongezeka iwapo watapata ushirikiano wa wananchi wanaofanya shughuli zao ndani ya bahari. Aidha, alisema itaandaa utaratibu maalumu kuhakikisha mapato ya nchi hayapotei kiholela na kila kampuni kuona inalipa kwa mujibu wa sheria.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk.Aboud Sulaiman Jumbe alisema hifadhi ya bahari ni muhimu kwa mazingira ya nchi na ndiyo chachu ya falsafa ya uchumi wa buluu na maendeleo yake.

Alisema mkataba huo utaongeza mnyororo wa thamani pamoja na pato la taifa na itakuwa na chanzo chake kipya cha mapato.

Mwakilishi kutoka Kampuni ya Beyond, Jane Brack, alisema kuwa ushirikishwaji huo unaenda kutoa tija za utunzaji wa mazingira katika maeneo ya bahari ya Kisiwa cha Mnemba.

# Hospitali yaomba msaada chakula kufuturisha wagonjwa, madaktari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Idara ya Mipango Hospitali ya Mnazi Mmoja Zanzibar, Abdallah Khamis Haji, amesema hospitali hiyo inauhitaji wa chakula hasa katika mwezi huu wa Ramadhani kwa ajili ya wagonjwa na madaktari hospitalini hapo.

Aliyasema hayo jana ofisini kwake baada ya kupokea msaada wa vyakula mbalimbali kutoka taasisi ya Vigor Zanzibar.

Alisema, ingawa uongozi wa hospitali hiyo umeweka bajeti kwa ajili ya chakula lakini bado wanauhitaji.

"Kutokana na uhaba wa watalamu wa afya wapo baadhi ya madaktari ambao wanafanya kazi kwa zaidi ya saa 12, hivyo msaada huu utasaidia kwa wagonjwa wetu na madaktari kupata chakula hasa kipindi hiki cha Ramadhani"alisema.

Aidha, alisema wakijitokeza wahisani kujitolea kusaidia inawaongezea nguvu badala ya kupata chakula kidogo cha futari ikiwezekana kupata na chakula cha daku.

Balozi wa taasisi hiyo, Khaitham Salum Turkey, alisema wameamua kutoa msaada huo kwa sababu madaktari wanafanya kazi muda mwingi wakiwa hospitalini hapo na wanahitaji chakula cha kufuturu.

Alisema, chakula hicho siyo kwa ajili ya madaktari pekee pia kwa wagojwa waliolazwa hospitalini hapo wakiendelea kupata matibabu.

Taasisi hiyo pia, ilitoa msaada huo wa chakula kwa nyumba ya kurekebisha tabia kwa vijana walioacha matumizi ya dawa za kulevya iliyopo Bububu Unguja na kwa watoto yatima wa Shehia ya Chuwini visiwani humo.

Msimamizi wa nyumba hiyo, Fauzi Khamis alisema wanaishukuru taasisi hiyo kwa msaada huo wa chakula akisema itapunguza changamoto inayowakabili ya kumudu gharama za uendeshaji ikiwamo chakula.

Sheha wa Chuwini, Muhammed Shehe Kheri, alisema msaada huo utasadia familia zenye watoto yatima ili kupata chakula hasa katika kipindi hiki cha Ramadhani na kuzitaka taasisi zingine kuzifikia familia zenye mazingira magumu na watoto yatima ili kujisikia faraja.



Katibu wa Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu Taifa (NEC), Idara ya Itikadi na Uenezi CCM Zanzibar, Khamis Mbeto Khamis (wa pili kushoto), akikagua samaki aina ya pweza, katika soko la Darajani Zanzibar, wakati wa ziara yake ya kuangalia hali ya upatikanaji wa chakula kisiwani humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Serikali kuimarisha miradi ya maendeleo Pemba

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Zanzibar imesema inaendelea na dhamira yake ya kupeleka usawa wa maendeleo kisiwani Pemba katika nyanja zote ikiwamo kuimarisha miundombinu ya barabara na ujenzi wa uwanja wa ndege wa kimataifa.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi aliyasema hayo Ikulu Zanzibar wakati akifanya mazungumzo na Balozi wa Uingereza nchini Tanzania, David Concar, Ikulu Zanzibar.

Dk. Mwinyi, alisema serikali imedhamiria kuifungua Pemba kwa maendeleo makubwa baada ya kukamilika kwa ujenzi mpya wa uwanja wa ndege wa kimataifa ili kuweka uwiano sawa na mandhari ya Kisiwa cha Unguja kwa kuondoa utofauti wa maendeleo uliopo baina yao.

"Kimaendeleo Unguja na Pemba hazipo sawa tunataka kuibadilisha Pemba kuwa sawa na Unguja kimaendelo," aliahidi Dk. Mwinyi.

Aidha, alisema ujenzi wa barabara kutoka Chakechake hadi Mkoani na Ujenzi wa uwanja wa ndege mpya kwa sasa ni miradi mikubwa ya maendeleo kisiwani humo ambayo ni muhimu kwa Zanzibar.

Dk. Mwinyi alisema tayari serikali imefikia hatua nzuri ya mazungumzo baina yao na wakandarasi wa ujenzi huo .

Alisema, kukamikika kwa miradi hiyo kutaifungua zaidi Pemba kimaendeleo kwa kuruhusu ndege kubwa za kimataifa kutua kisiwani humo.

Balozi David Concer alisema dhamira ya Uingereza kwa Serikali ya Zanzibar ni katika ushirikiano wao wa miradi hiyo iliyopo Pemba.

Alisema mchakato wa fedha upo na kusisitiza matarajio yake ya kuanza haraka kwa ujenzi huo.

Aidha, Balozi Concer alimuahidi Rais Mwinyi kwamba Serikali ya Uingereza wataendeleza ushirikiano uliopo katika kukuza sekta za maendeleo na kuimarisha uhusiano wao kidiplomaisia uliopo baina ya nchi hizo.



**RAYVANNY**

UKURASA 14

Nipashe MWANGA WA JAMII

BT BURUDANI TELE

JUMAMOSI APRILI 1, 2023



# HAPO INATOSHA

MAUA Sama ni mmoja wa wasanii wa kike nchini ambaye hana mambo mengi katika njia ya kujiongezea umaarufu.

Kutokana na tabia yake hiyo, amekuwa akijiepusha na mambo mbalimbali yanayofanywa na wasanii maarufu wa muziki, hasa kujichora mwilini maarufu kama tattoo.

Mwili wa Maua Sama umekuwa na mwonekano wa kiasili, kiasi ambacho kila nguo anayovaa au pambo analotumia linamkaa vyema.

Hata hivyo, hivi karibuni mwanamuziki huyo ameibua mjadala mkali baada ya kuwaomba mashabiki zake kumsaidia kutaja sehemu gani ya mwili wake anaweza kuchora Tatoo. Hata hivyo, mashabiki wengi walimtaka kuacha kufuata mkumbo na badala yake kusimama kama alivyo, kwani mwonekano wake ni utambulisho tosha.

Mmoja wa mashabiki hao alimtaka kutokurupuka na kujichora tatoo, kwani jinsi alivyo sawa na anakubalika.

"Usiweke, uko vizuri na upo wa kipekee jinsi ulivyo, msanii pekee wa Tanzania asiye na uchafu mwilini mwake, heshima kubwa sana," ameandika mmoja wa mashabiki hao.

Wanamuziki wengi wamejichora tattoo katika miili yao, lakini wataalamu wanaonya kwamba

BASI SAWA

## Chuchu kwa hili huwezi



MWIGIZAJI na mtayarishaji wa filamu nchini, Chuchu Hans, amesema amekumbana na matatizo mengi wakati akiandaa tamthilia ya Jeraha, mpaka ilipokamilika.

Amesema moja ya tatizo lilokuwa likimsumbua ni kumpa nafasi baba mtoto wake Ray Kigosi, ili aweze kushiriki kwenye tamthilia hiyo.

Chuchu amedai kuwa kwa sasa wawili hao hawana uhusiano wa kimapenzi, badala yake wanasaidiana wanalea mtoto wao na kufanya kazi pamoja.

## Ali Kiba hatakagi hasara



MFALME wa muziki wa Bongo Fleva, Ali Kiba, anafikiria kuacha kuimba nyimbo za mahaba kuto-kana na kumfilisi kifedha.

Akizungumza ka-tika kituo cha redio cha East Africa,Ali Kiba amesema kwamba yeye ameanza kufanya video za muziki wa kuchezeka ili kupunguza zinazotokana na kuwekeza katika video za nyimbo za mapenzi ambazo hazimpi faida.

"Ni kweli tunafanya video lakini ukweli video zina-chukua pesa nyingi sana kwa wasanii, na wanasubiri pesa zirudi. Unajua muziki ni biashara, mimi nimejaribu kufanya mwaka huu lyrics video au hata dance video ili waone jinsi nilivyoimba muziki wangu kupitia huko," alisema Alikiba.

## Baba Levo amfariji Diamond



MWANAMUZIKI na mchekeshaji, Baba Levo, amesema kuna hujuma zimefanyika na kusaba-bisha bosi wake Diamond Platnumz, kutoingia katika orodha ya wanamuziki wanaopendwa na Makamu wa Rais wa Marekani, Kamala Harris.

Baba Levo ameeleza Diamond ndio msanii pekee kutoka Tanzania anayesiki-lizwa zaidi huko Marekani hivyo anashangazwa kuona jina lake limekosekana.

Ameongeza kuwa kwa upande wake yeye anahisi kuna mchezo wa kisiasa ambao umeleta maajabu hayo.




# Rayvanny majigambo mengi

MWANAMUZIKI na CEO wa lebo ya muziki ya Next Level, ametoboa siri yake ya kutumia zaidi ya milioni 70, kwa ajili ya kurekodi video ya wimbo wake mpya.

Mkali huyo amesema kwa siku saba alikuwa akichukua picha ya video hiyo na kila siku ilimgharimu kiasi cha shilingi milioni 10.

Amesema anatarajia wimbo huo utawaunganisha mashabiki zake kutokana na kuwa kali na ubora unaokubalika kimataifa.



# Akothee haambiwi kitu kwa mzungu

MWANAMUZIKI mwenye vituko kutoka Kenya, Esther Akoth, almaarufu kama Akothee, amefichua kwamba kuna uhusiano mzuri kati ya watoto wake watano na mchumba wake Omosh.

Akizungumza hivi karibuni, amesema kuwa mpenzi wake huyo mzungu anaelewa jinsi ya kuwasiliana vizuri na watoto wake.

"Watoto wangu wanampenda, wan-ampenda sana. Omosh anajua jinsi ya kushughulikia watoto wangu," amesema.

Hata hivyo, mwanamuziki huyo mwe-nye umri wa miaka 43 alifichua kwamba watoto wake huwa hawamuiti mpenziwe 'baba'.

## 5 ZINAZOMNOGESHA HAYATI BOBO SUKARI

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Afrika na dunia nzima ilikuwa ikiomboleza kifo cha mwanamuziki mpiga gitaa la kati rhythm, Lokasa ya Mbongo, mashabiki wa muziki ukanda wa Afrika Mashariki ulipata pigo baada ya kuondokewa na mmoja wa waimbaji bora kuwahi kufika nchini Tanzania, Bobo Sukari.

Mwanamuziki huyo mwinbaji wa sauti tamu ya kwanza, alifariki dunia ghafla usiku wa kuamkia Machi 20 nyumbani kwake Mwananyamala, jijini Dar es Salaam kwa kile kilichota-jwa kuwa ni shinikizo la damu.

Kwa mujibu wa mchumba wa Bobo, ambaye ni binti wa kiongozi wa zamani bendi ya Maquis Original, Mbuya Ma-konga Adios alisema mwanamuziki huyo hakuugua chochote kabla ya umauti.

"Bobo alikuwa mzima kabisa na amefanya shughuli zake kama kawaida, lakini alipoenda kujipumzisha ndiyo ikawa hivyo," alisema binti huyo.

Bobo ambaye alirejea Tanzania mwaka jana kutoka Sweden alikokuwa akiishi na kupiga muziki kwa muda mrefu baada ya kuondoka Maquis Original yeye na Dekula Kahanga vumbi, mwishoni mwa miaka ya 1990.

Jina lake halisi ni Luhembwe Mwanavita, lakini Bobo Sukari lilikuwa ndiyo jina lake la kimuziki, akiwa mzaliwa wa Kisan-gani Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, na hadi anafariki alikuwa na miaka 67.

Alihamia nchini mwaka 1990 na kujiunga na bendi za Carni-val na Lulu, kabla ya mwaka 1991 kujiunga na Maquis Original na kuichangamsha sana akiwa na wenzake wawili ambao ni marehemu Fredito Butamu na Kivukutu wakitumia mtindo ulioondokea kuwa maarufu wa 'washawasha'.

Alizikwa kwenye makaburi ya Kinondoni jijini Dar es Salaam. Hizi ni baadhi ya nyimbo zake tano bora alizowahi kuimba akiwa Maquis.

**'BABA WILLY'**

Wimbo huu ulitungwa na mwamuziki Kaumba Kalenga, lakini marehemu Bobo Sukari alikuwa mmoja wa waliouimba kwa ustadi wa hali ya juu.

**'MSAADA SIYO DENI'**

Ni moja kati ya nyimbo zilizopendwa miaka hiyo alipoji-unga, na yeye mwenyewe sauti yake inasikika vizuri kwenye wimbo huo, kwani kuna vipande alipamba peke yake.

**'NTUMBA'**

Ulitungwa na Tshimanga Kalala Assosa, lakini ukaimbwa kwa ustadi mkubwa na Bobo Sukari kwa kupokezana na mwenzake huyo kwa lugha ya Kilingala.

**'MAYANGA'**

Ni moja kati ya nyimbo maarufu za Maquis Original ambazo marehemu aliziimba na umempatia umaarufu mkubwa.

**'SULTAN QABOOS'**

Tofauti na nyimbo nne za juu zilikuwa na Maquis Original, wimbo huu uliimbwa na Bobo Sukari akiwa nchini Sweden na Dekula walipoondoka nchini Tanzania. Ulikuwa ni maalum kwa kumsifu mfalme aliyetawala nchi ya Oman kuanzia mwaka 1970 hadi alipofariki dunia mwaka 2020 Qaboos bin Said Al Said. Uliimbwa kwa lugha ya Kiarabu na hadi leo ni mtamu mno masikioni kuusikia, hasa sauti ya Bobo.



# Bado nadanga: Utamu wa ndoa iliyoyeyuka

**Na Adam Fungamwango**

MTAKA yote hukosa yote, na mtaka nyingi nasaba hupata mwingi msiba. Ni methali za watu wa zamani waliokuwa na hekima.

Walikuwa na maana kuwa siku zote ukitaka mambo mawili mazuri kwa wakati mmoja ni tabu hutapata kutokana na asili ya dunia jinsi ilivyo. Acha moja, tafuta moja. Nyingine ina maana mtu yeyote mwenye ndugu wengi, kwake inakuwa ni rahisi kupata matatizo mengi kutokana na wingi wa ndugu alionao.

Kesho ataambiwa huyu anaumwa, kesho yule ana tatizo fulani, kesho kutwa msiba, hii ni tofauti na mwenye ndugu wachache.

Mifano hii inakwenda kwenye hali halisi ya dunia. Hebu tuiangalie filamu hii yenye mafundisho makubwa. Inaitwa 'Bado Nadanga.'

Baadhi ya wasanii waliocheza ni Verena Mathayo, Nassor Chilumba, Rayuu Chande, Hawa Ramadhani na wengineo.

Nassor na Radhia ni wapenzi wa muda mrefu na wapo kwenye mikakati ya ku-funga ndoa. Nassor akamwambia Radhia kuwa yeye tayari amekamilisha kila kitu, hivyo anataka ajiandae kwa hilo.

Radhia anaruka futi mia. Anamwambia mpenzi wake kuwa kwa sasa hana mpango wa kuolewa na waendelee tu kuwa wap-enzi.

Akaulizwa sababu akasema majukumu ya ndoa anayajua, hivyo hayupo tayari kwa sasa. Akili yake iliienda mbali. Ujana atamuachia nani? Kudanga nako je? Bado anadanga, hivyo akiolewa itakuwa ni kama kifungo.

"Kama unataka kuoa, basi tafuta mwan-amke mwingine, siyo mimi, kama unataka kunioa mimi, subiri nikiwa tayari nitak-wambia.

Nassor akaamua kufanya kama alivy-oambiwa. Akatafuta mwanamke mwingine



akaoa.

Siku zikapita sasa Radhia akawa anaita-ka ndoa. Wa kumuoa hakuna. Akamtafuta Nassor na kuanza kumlaumu kwa nini ameoa mapema? Nassor akamkumbu-sha alivyokuwa anambembeleza lakini akakataa.

Moyo wa Radhia ukavunjika, akaapa kuisambaratisha ndoa yenyewe hadi yeye arejee kwenye mamlaka.

Akatinga nyumbani kwa mke wa Nassor na kumwambia kuwa yeye ni msichana mzuri mdogo, kwa nini ameamua kuolewa mapema vile. Akamshawishi aondoke kwa mwanaume. Pia akamwambia mumewe ni mhuni na ana wanawake wengi.

Akarejea kwa Nassor na kumwambia mkewe anamsaliti na amemfuma laivu na mabwana.

Ameshakaanga mbuyu, anawaachia wenye meno watafune. Nassor na mkewe Shakira wanaanza kushutumiana. Lakini shoga yake Shakira, Tunu anaufahamu mchezo mzima kwa sababu ana ubia na Radhia. Ni yeye ndiye aliyemfuata mmoja mmoja, Nassor na Shakira na kuwaambia kuwa anayewagombanisha ni Radhia.

Ndipo Nassor anapomueleza mkewe kuwa kabla yake alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Radhia, lakini ngoja ngoja yake ndiyo iliyomfanya amuoe yeye na wala kwa sasa si mpenzi wake kama ilivy-okuwa inavumishwa.

Mke naye akamwambia mumewe kuwa hana mabwana nje, na yote ni uchokonozi wa Radhia ambaye huko nyuma alishawa-hi kumfuata kutaka aondoke.

Baada ya kujulikana njama zake, Radhia anakwenda kuomba radhi kwa Nassor na mkewe akiapa hatorudia tena.



## Kama kweli ni kheri

MKALI wa Afrobeats David Adeleke, maarufu kama Davido, amethibitisha kuwa amemuoa mpenzi wake, Chioma Rowland.

Mwimbaji huyo alithibitisha hayo katika mahojiano na mwanahabari Kiekie, amesema ukimya wake ulikuwa na mambo mengi ikiwamo harusi yake na Chioma.

Kulingana na Davido, alipumzika na kujiondoa katika mitandao ya kijamii baada ya kumpoteza mwanawe, Ifeanyi, na kuhitaji muda wa kutafakari.

"Sijawahi kuchukua mapumziko ya aina hii. Ilikuwa wakati wa kupumzika, kutafakari, muda mwingi wa familia, Tayari nilikuwa na ziara, nilisafiri na kuoa." alisema.



## Portable umeshindikana

JESHI la Polisi nchini Nigeria, linamchunguza mwanamuziki Habeeb Okikiola, maarufu kama Portable, kwa madai ya kuwatukana polisi walioko kazini.

Msemaji wa Kikosi hicho, CSP Olumuyiwa Adejobi, alithibitisha hilo katika taarifa yake aliyoitoa juzi.

Adejobi alilaani kitendo cha mwanamuziki huyo kwa kuweka video mtandaoni, ambapo alionekana akiwatolea maneno machafu askari polisi ambao walikuwa wanatekeleza wajibu wao wa kisheria.

Alisema kuwa kitendo chake kilikuwa cha uhalifu na kinaadhibiwa kwa sheria za uhalifu za nchi hiyo.

## Whitemoney huo ni ushauri tu

MSHINDI wa Big Brother Naija, 'Shine Ya Eyes', Whitemoney, amedai kusumbuliwa na washiriki wenzake wa kike ambao wanatafuta wanaume matajiri.

Whitemoney amesema kuwa wanawake wengi kwenye shoo hiyo, baada ya kuondoka, wanakuja kwake ili kuwaunganisha na marafiki zake matajiri.

Mwimbaji huyo alifichua kuwa wengi wa wanawake wa rika lake huingia kwenye shindano hilo la televisheni ili kujitangaza badala ya kutafuta fursa.





## Mercy yote kuomba toba

MWIGIZAJI kutoka Nollywood Mercy Aigbe, amezungumzia uzoefu wake wa kuwa mke wa kiislam katika kipindi hiki cha mwezi wa Ramadhani.

Aigbe, ambaye ni mke wa pili wa mfanyabiashara Kazeem Adeoti, alisema ni wajibu wake kuamka asubuhi kwa ajili ya kuandaa futari ya jioni.

Msanii huyo amefafanua kwamba anakabiliana na uchovu wa swaumu, hata hivyo bado anahangaika kuwaandalia wanafamilia futari nzuri.

## Marley mwezi Ramadhani umekubadilisha

MWANAMUZIKI anayependwa na vijana wa mitaani, Naira Marley, amewahimiza waumini wa Kiislam, kuacha michezo ya kamari wakati wa mfungo wa mwezi wa Ramadhani.

Mwimbaji huyo aliandika haya kupitia ukurasa wake wa Twitter, ambapo alionya mashabiki zake kuacha kucheza mchezo huo ambao ni kinyume na imani yao.

Amesema kipindi hiki kimetengwa kwa ajili ya kujiepusha na chakula, vinywaji, kuvuta sigara, na ngono ili kuboresha uhusiano wa mtu pamoja na Mungu.







## Maofisa ugani wilaya tatu wakabidhiwa pikipiki

**Na Oscar Assenga,** TANGA

SERIKALI mkoani Tanga imekabidhi pikipiki 198 kwa ajili ya maofisa ugani wa Wilaya ya Lushoto, Handeni na Korogwe, huku ikielekeza zitumike kutoa huduma kwa wakulika.

Kaimu Mkuu wa Mkoa huo, Hashimu Mgandilwa alitoa agizo hilo alipomwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba katika makabidhiano ya pikipiki hizo.

Mgandilwa aliwaagiza maofisa ugani hao kwamba wasizigeuze pikipiki hizo kama bodaboda, bali wawafikie wakulima kwa wakati na kuwaelimisha kulima kilimo chenye tija

"Ni marufuku kumpa pikipiki mtu yeyote yule ambaye hausiki, hizi pikipiki zimenunuliwa kwa fedha ya umma, hivyo mnatakiwa mzitunze na kuzihifadhi sehemu nzuri. Msizigeuze kama bodaboda, ama msizitumie kwa mambo ya anasa, tumieni kwa masilahi ya wananchi na taifa,"alisema

Mgandilwa aliwataka maofisa hao kuhakikisha kuwa kilimo kinachangia asilimia 10 katika pato la taifa ufikapo mwaka 2023.

Kadhalika, alisema lengo la kutolewa vitendea kazi hivyo ni kuimarisha kilimo biashara.

Alisema kuimarisha huko kilimo biashara ni kulisaidia taifa kupata tija na manufaa kwa wakulima, ikiwamo kuimarisha uchumi wa nchini kupitia kwenye sekta hiyo.

Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Tanga, George Mbaga, alisema kuwa mkoa huo unapaswa kupokea pikipiki 377, lakini awamu ya kwanza Wizara ya Kilimo, imewapa pikipiki 198.

Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika wa Wilaya Handeni, Chiza Kamele, alisema pikipiki hizo zinakwenda kumaliza tatizo la uhaba wa vitendea kazi kwa maofisa ugani ngazi ya kata na vijiji.

# DC aagiza viongozi kata, kijiji kusimamia uhifadhi chakula

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

MKUU wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Dk.Suleiman Serera, amesema angalizo lake kuhusu umuhimu wa wananchi kuhifadhi akiba ya chakula walichonacho linapaswa kutekelezwa na viongozi wote kuanzia ngazi za vitongoji, vijiji na kata.

Kwa mujibu wa Dk. Serera angalizo hilo linalenga kuhakikisha wananchi wa wilaya hiyo wanapambana na baa la njaa kwa kuwa na uhakika wa usalama wa chakula.

"Tunzeni sana chakula mlichonacho, kwa sababu kwa zaidi ya miaka mitatu sasa wilaya yetu imekumbwa na ukame. Narudia, suala la usalama wa chakula ni muhimu katika maeneo yetu,"alisema

"Simanjiro tujipange sasa kwa mazao ya kuhifadhi ghalani, iwe ni mahindi, maharagwe, vitunguu maji, alizeti au mengineyo, tukakae na wakulima na kujadili hili,"alisema Serera.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Samwel Gunza, alisema suala la kuwapo kwa stakabadhi ghalani ni jambo muhimu kwa wakulima, hivyo wanapaswa kutekeleza.

"Stakabadhi ghalani itawasaidia wakulima kwa kuwa kule Mtama mkoani Lindi nilikuwa mkurugenzi kabla sijahamia Simanjiro, walifanikiwa kuwaepuka walanguzi maarufu kama kangomba,"alisema Gunza.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Baraka Kanunga, alisema uwepo wa mizani katika minada kutasaidia tija kwa wafugaji na wakulima kwa kuwa watapima kwa uhakika mifugo yao.

"Mnapokuwa na mizani kwenye minada kutamnufaisha mfugaji kwa kuwa atatambua ng'ombe wake ana kilo ngapi na siyo kupima kwa macho na mkulima atabaini uzito wa mazao yake badala ya rumbesa,"alisema Kanunga.

Diwani wa Kata ya Terrat, Jackson Materi, alisema kufanyika kwa biashara kwa njia ya mtandao ni jambo zuri kwa kuwa wakulima au wafugaji wanaweza kuuza mazao yao bila kuonana na mnunuzi.

"Japokuwa hilo litakuwa jambo geni hapa kwetu Simanjiro ila ni zuri kwa kuwa dunia inakwenda kasi mno kwa kuwa kupitia mtandao mnaweza kufanya biashara bila kuonana,"alisema Materi.

Hata hivyo, Meneja Mipango na Uhamasishaji wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi Ghalani, Sura Ngatuni, alisema sasa hivi walanguzi wanaingia shambani na kurubuni wakulima, hivyo wanapaswa kupewa elimu ya stakabadhi ghalani ili wahifadhi mazao yao na kubakiza ya kutumia.

"Mfano, mtu amelima gunia zake 100, anapaswa kujipanga kuwa ataweka ya chakula gunia ngapi za kula na familia na nyingine ahifadhi ghalani na kuepuka kurubuniwa na walanguzi,"alisema Ngatuni.




Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Balozi Dk. Batilda Buriani (kulia), akipokea msaada wa moja ya kompyuta na vifaa vingine vya TEHAMA vyenye thamani ya Sh. milioni 150 kutoka kwa Meneja Mauzo Mwandamizi wa Vodacom Tanzania Plc Kanda ya Ziwa, Ahmed Akbarali (katikati) katika Shule ya Sekondari Kariakoo, mkoani humo, kwa ajili ya shule za sekondari 20, ikiwa ni sehemu ya mradi wa uunganishwaji wa shule za sekondari unaolenga kuziunganisha shule 300 Tanzania kwa kushirikiana na 'African Child Projects' na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF). Kushoto ni Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Tabora, Neema Kapesa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Warioba ataka utafiti uendane na mabadiliko tabianchi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Jaji Mstaafu Joseph Warioba, amewataka wajumbe wa baraza la chuo hicho kuhakikisha utafiti unaofanywa kuhusiana na misitu, kilimo na uvuvi, unaendana na mabadiliko ya tabianchi ili uweze kutatua matatizo yanayotokana na mabadiliko hayo.

Jaji Warioba ambaye aliwahi kuwa Waziri Mkuu aliyasema hayo jana Jijini Arusha wakati wa kufungua mafunzo yaliyowahusisha wajumbe wa baraza la chuo hicho.

Mafunzo hayo yalifanyika katika Msitu wa Mafunzo wa Olmotonyi uliopo chini ya Ndaki ya SUA.

Pamoja na mambo mengine, mafunzo hayo yaliambatana na uzinduzi wa mashine ya kuchakata mazao ya msitu aina ya Slidetec Sawmill 2020 yenye thamani ya Sh.milioni 200.

Alisema tafiti zao wanazofanya lazima ziendane na mabadiliko ya tabianchi, ili kuleta tija na kasi ya maendeleo kutokana na hali halisi ya mazingira.

"Lakini nasisitiza nidhamu katika matumizi ya fedha, pamoja na ufanisi wenye tija na weledi katika kuchochea maendeleo ya chuo hiki.

"Mafunzo yanayotolewa yawabadilishe katika kuleta ufanisi zaidi sanjari na kuwa na nidhamu ya fedha, lakini nawapongeza kwa kununua mashine hii ya kisasa, inayotoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi katika sekta za misitu,"alisema.

Makamu Mkuu wa Chuo cha SUA, Prof. Raphael Chibunda, alisema kuwapo wa mashine hiyo kumesaidia kuboresha mafunzo na kuwa ya kisasa kwa vitendo. Mashine hiyo ina uwezo wa kuchakata mita za ujazo 10 hadi 15 kwa saa nane, tofauti na awali ambapo kulikuwapo na mashine ya mbao inayochakata mbao mita za ujazo 5 hadi 7 kwa saa 11

Alisema msitu huo wa mafunzo ya Olmotonyi unasaidia pia uhifadhi wa Mlima Meru na kwa mwaka mapato ya Sh. milioni 700 hadi Sh. bilioni moja hupatikana kutegemea na miti ilivyokuwa. Pia, hutoa ajira kwa vibarua zaidi ya 60 katika msitu au katika kuchakata mbao na wanufaika wakubwa wananchi wanaozunguka msitu.

Kaimu Rasi wa Ndaki ya Misitu, Wanayamapori na Utalii, Dk. Agnes Shirima, alisema mashine hiyo mpya iliyozinduliwa lengo ni kuongeza uzalishaji ikiwemo kufundisha wanafunzi wa shahada ya misitu na wale wanaochukua teknolojia ya misitu na uongezaji wa samani.

Alisema chuo kilikuwa na mashine mbili aina ya Kara, iliyonunuliwa mwaka 1981 na Laimet 1998 zenye uwezo wa kuchakata mbao ujazo wa mita tano hadi saba kwa saa.

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Kutana na jitu lishibalo, Power Mabula

## - Alizuia gari kwa mikono, bodaboda kwa nywele, jiwe kuvunjwa kifuani

**Na Adam Fungamwango**

UNAFUNGUA gazeti, unakutana na picha ya mtu mmoja mrefu, aliyejengeka vema na kujaa misuli mikononi na kifuani. Mtu huyo ana nywele nyingi zenye rasta mbili ndefu, kiunoni hadi kwenye mapaja amevaa kitu mfano wa ngozi, akijifunga mithili ya msuli mfupi mgumu na kuacha eneo kubwa la mwili wake wazi. Chini alikuwa amevaa viatu virefu kuanzia chini hadi karibu kabisa na magoti.

Halafu unakutana na maandishi ya 'Kutana na jitu lishibalo Power Mabula.'

Lilikuwa ni tangazo la mbabe huyo likionyesha ni wapi siku hiyo atafanya maonyesho yake. Huyu ndiye Power Mabula ambaye hakuna mtoto, mzima, au kijana wa kuanzia miaka ya mwanzoni mwa 1980 hadi mwanzoni mwa 1990 ambaye hamfahamu.

Alikuwa maarufu sana kwa michezo ya kutumia nguvu. Baadhi walimuona laivu akifanya maonyesho hayo, akizunguka Tanzania nzima. Wengine walimsoma na kuona picha zake kwenye magazeti na wengine wakasimuliwa na waliomuona.

Alikuwa na uwezo wa kuizua gari aina ya Land Rover lisiondoke, akitumia kamba kubwa ya katani au mnyororo kuizuia. Alikuwa pia ana uwezo wa kuzuia magari mawili aina ya na 404 Peugeot au 505 wakati huo yasiondoke kwa wakati mmoja, mmoja ilifungwa upande huu na lingine upande mwingine, yeye akiwa katikati. Wakati mwingine aliweza kulivuta gari kwa kamba akitumia meno.

Power Mabula pia, alikuwa na uwezo wa kuizuia pikipiki ishindwe kuondoka kwa kutumia nywele zake. Akifunga kamba ilifungwa kwenye pikipiki kwenye rasta zake, huku mwendashaji akijitahidi kutia gia na kuondoka, lakini wapi.

Jitu hilo, pamoja na michezo mingi, ikiwemo kubeba mifuko kadhaa ya simenti kwa kutumia meno, alikuwa na uwezo wa kupitisha gari kifuani kwake, bila kupata madhara yoyote.

Usisahau pia na kuvunjiwa jiwe kubwa kama yale yanayopatikana Kunduchi kifuani kwa kutumia nyundo. Aliweza pia kunyanyua matofali kadhaa makubwa yaliyofungwa kwa kamba, akitumia meno.

Ilikuwa ni kitu cha hatari kukiona, lakini ni kama watu walikuwa hawaamini macho yao, lakini ni kweli mwamba huyo alikuwa anafanya kwa malipo madogo tu wakati huo, kwani hata wanafunzi walikuwa na uwezo wa kwenda kulipa na kuangalia michezo hiyo.



Wakati mwingine aliweza kufika hadi mashuleni na kufanya michezo yake hiyo.

Huyu ndiye aliyekuwa mchezaji wa kutumia nguvu maarufu zaidi nchini Tanzania wakati huo.

Baadaye walikuja wengine, lakini hawakuweza kumfikia mwamba huyu, kwa kile alichokuwa akifanya kwenye maonyesho yake na hata umaarufu.

Baadaye kukaja michezo ya kupigana, maarufu kama mieleka. Power Mabula yeye hakujishughulisha kabisa na michezo hiyo. Yeye aliendelea na michezo yake ya nguvu tu ambayo baadaye ilianza kushuka chati, michezo ya mieleka nafasi yake.

Ikaanza kutoa wanamieleka wazuri na waliotokea kuwa maarufu nchini Tanzania wanaokumbukwa mpaka sasa.

Kwanza walitaka kupigana, matangazo yanaanza kutoka kwenye magazeti. Kunakuwa na picha zao, halafu kila mmoja anampa 'mkwara' mwenzake.

Yale maneno wanayotishana ndiyo yanayovuta mashabiki wengi kujazana kwenye kumbi mbalimbali kushuhudia mapambano yao.

"Njoo na jeneza kabisa, hautorudi nyumbani ukiwa hai". Mwinngine naye anajibu "Leo nitakutwanga hadi ndugu zako wakuulize, umegongwa na treni au umepata ajali ya ndege kuanguka na wewe ukiwemo?"

Haya yalikuwa ni baadhi ya maneno ambayo mashabiki na wasomaji walikuwa wakiyapenda sana kuyasoma kwenye gazeti kabla ya mapambano.

Kuna mtu aliniambia siku hizi michezo hiyo haipo kwa sababu kila mtu anataka kujifanya 'sharobaro.



Akasema, hata wale wachache wanaokwenda 'gym' wanafanya hivyo ili watishe na kupiga watu mitaani, wakae milangoni kwenye kumbi ya starehe au kwenye vituo mbalimbali vya mabasi kwa ajili ya kukatia watu tiketi.

Baadhi ya wanamieleka maarufu waliopata kutokea nchini ni Power Vuru Mroma, Power Bukuku 'Sumu ya Mamba', Power Savimbi, Power Tx Chaka, Power Banardo 'Tai Kichaa', Power Ngeta 'Super Kibonge', Power Iranda, Power Mwanakulya.

Wengine ni Power Sangandele, Power Nyati, Power Mwanza, Power Nassor, Power Liston Dudu na Power Masai ambaye ni mmoja wa waanzilishi wa michezo hii ya mieleka nchini.

Mmoja wa wanyanyua vitu vizito ambaye ameshastaafu na hakutaka jina lake lichapishwe, alisema hakuna ushirikina wowote kwenye mchezo huo wa kutumia nguvu isipokuwa ni sayansi ya akili na nguvu ndiyo inayosababisha waonekane wao ni watu tofauti.

Anasema, ndiyo maana hakuna aliyesikia 'power' yoyote anapitisha lori kifuani kwake, mara zote ni magari ya kawaida kama vile Land Rover na magari mengine madogo ambayo yanaendana na uzito wa mhusika.

Kuhusu chakula alisema kulikuwa na uvumi kuwa wanakula chakula kingi zaidi kama vile mbuzi mzima peke yao na kilo tano za ugali, kitu ambacho si kweli.

"Huo ni uroho. Power anakula chakula cha kawaida ambacho wengine wanakula, ila anashauriwa ale nyama kwa wingi, mboga za majani, mahagare, japo atakula kwa kipimo cha juu zaidi kwa sababu anafanya kazi za nguvu na mazoezi magumu, lakini si kwa kiwango kinachozungumziwa mtaani. Maharage na mboga za majani zinajenga na kulinda mwili na hiyo ndiyo inashauriwa zaidi," alisema Power huyo ambaye kwa sasa ni mwanajeshi Mstaafu. Unafahamu nini kuhusu watu hawa wa kazi?

**Tuma meseji 0716 350534**



# Finland ruksa kujiunga Nato

**HELNSIKI,** UJERUMANI

NCHI ya Finland itakuwa mwanachama wa 31 wa Jumuiya ya kujihami ya mataifa ya Ulaya (Nato) baada ya bunge la Uturuki kupiga kura kuidhinisha ombi lake.

Uturuki ilikuwa imechelewesha ombi la Finland, la kujiunga na muungano huo, kwa miezi kadhaa ikilalamikia taifa hilo la Nordic kuunga mkono magaidi.

Sweden, ambayo iliomba kujiunga na Nato, mwezi Mei mwaka jana, bado inazuiwa kutokana na malalamiko kama hayo.

Upanuzi wowote wa Nato unahitaji kuungwa mkono na wanachama wake wote.

Finland sasa itakubaliwa rasmi kujiunga Nato katika mkutano wake utakaofanyika Julai nchini Lithuania.

Katibu Mkuu wa Nato, Jens Stoltenberg, alisema kwenye Twitter kuwa anatarajia kuinua bendera ya Finland katika Makao Makuu ya Nato katika siku zijazo.

Katika taarifa iliyotolewa kufuatia upigaji kura wa Uturuki, serikali ya Finland ilisema kujiunga na muungano huo kutaimarisha usalama wa nchi hiyo, na kuimarisha utulivu na usalama katika eneo hilo.

“Kama washirika, tutatoa na kupokea ulinzi. Tutalindana. Finland inasimama na Uswidi sasa na siku zijazo na inaunga mkono maombi yake,” Waziri Mkuu Sanna Marin aliandika kwenye Twitter.

Rais wa Uturuki Recep Tayyip Erdogan, aliidhinisha ombi la Finland mapema mwezi huu, na kusifu hatua halisi na madhubuti za nchi hiyo kuhusu usalama wa Uturuki.

Lakini uadui wake unaoendelea dhidi ya Sweden ulikuwa wazi kwani aliishutumu tena nchi hiyo kwa kuwakumbatia wanamgambo wa Kikurdi na kuwaruhusu kuandamana katika mitaa ya Stockholm.

**BBC**



Msemaji wa kundi la waasi la M23, Meja Willy Ngoma (kulia) akikumbatiana na mwanajeshi wa Uganda kwenye eneo la mpaka la Bunagana jana. **PICHA: GETTY IMAGES.**

# Waasi M23 waondoka Bunagana

**KAMPALA,** UGANDA

WAASI wa M23 wamesema wanaondoka katika mji wa Bunagana mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, na kuwaachia wanajeshi wa kulinda amani wa Uganda.

Msemaji wa kundi hilo Meja, Willy Ngoma, amesema kuondoka kwao katika eneo hilo la mpakani ni utekelezaji wa mazungumzo ya amani yaliyofanyika nchini Angola, mwaka jana.

Wanajeshi wa Uganda, walionekana wakivuka katika mji wa mpaka wa Bunagana juzi mchana.

Msemaji huyo wa kundi la M23, alisema mji huo ulikabidhiwa jana asubuhi.

“Waasi wanatekeleza makubaliano ya mikutano ya wakuu wa nchi na wakuu wa majeshi huko Luanda, Bujumbura na Nairobi,” alisema Meja Ngoma.

Bunagana ulitekwa na waasi Juni mwaka jana, iliwahi kuwa makao makuu ya kundi hilo ambalo linatakiwa kujiondoa katika maeneo yote ya Rutshuru, Masisi na Nyiragongo ambalo limekaliwa tangu mapigano yalipoanza tena mwaka jana. Katika taarifa ya Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, alisema wanajeshi wao wanaenda Bunagana kufanya kama jeshi lisiloegemea upande wowote huku Wakongo wakitumia muda huo kutatua matatizo yao ya kisiasa.

Burundi, Kenya tayari wamepeleka wanajeshi katika maeneo ambayo M23 wamekuwa wakiondoka, Sudan Kusini pia inatarajiwa kutuma wanajeshi.

Hali ya utulivu imetawala katika eneo lenye vita mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, ambapo zaidi ya watu laki tano wameyakimbia makazi yao.

**BBC**

# Papa Francis kutoka leo hospitalini

**ROMA,** VATCAN

KIONGOZI wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis anatarajiwa kutoka hospitalini leo na huenda akashiriki sherehe za wiki takatifu kuelekea maadhimisho ya Sikukuu ya Pasaka.

Hayo yamesemwa jana na mmoja wa makadinali wakuu.

Awali taarifa zilisema kwamba Papa alikuwa na usiku wa pili mtulivu hospitalini akipokea matibabu ya ugonjwa wa mapafu.

Vatican ilisema kiongozi huyo wa dini anaweza kula, kusali na kufanya kazi katika chumba chake maalum cha matibabu kilichoko ghorofa ya kumi ya hospitali ya Gemelli mjini Roma.

Awali ilikuwa imesemekana kwamba Papa Francis alipelekwa hospitali kwa ajili ya uchunguzi baada ya kulalamikia matatizo ya kupumua.

Hata hivyo, wahudumu katika hospitali hiyo walisema alikuwa ameambukizwa ugonjwa huo wa mkamba.

**DW**

# Odinga adai kunusurika kuuawa

**NAIROBI,** KENYA

KIONGOZI wa upinzani na waziri mkuu wa zamani wa Kenya, Raila Odinga, aldai kulikuwa na jaribio la kumuua baada ya gari lake kupigwa risasi saba siku ya Alhamisi wakati wa maandamano ya kuipinga serikali.

Katika kikao na wanahabari, Odinga alisema polisi walilenga gari lake na viongozi wengine wa upinzani wakati wa maandamano katika eneo la Eastlands, viungani mwa mji mkuu, Nairobi.

Pia alishutumu polisi kwa kuwalenga wanahabari wakati wa maandamano dhidi ya serikali na kudai kulikuwa na mipango ya kushambulia ofisi za Royal Media Services jijini Nairobi.

Odinga alikosoa jumuiya ya kimataifa kwa madai ya kupuuza ukiukaji wa haki za binadamu unaofanywa na mamlaka wakati wa maandamano hayo.

Alisema upinzani utafanya maandamano makubwa tarehe 3 Aprili kuishinikiza serikali kupunguza gharama ya maisha na kufanya mageuzi ya uchaguzi, miongoni mwa matakwa mengine.

Waandishi sita walijeruhiwa wakati wa maandamano ya Alhamisi, na kuongeza idadi ya wafanyakazi wa vyombo vya habari waliojeruhiwa kufikia 22 tangu maandamano hayo yalipoanza wiki iliyopita.

Hata hivyo, ubalozi wa Marekani umetoa masikitiko yake kuhusu kinachoendelea.

“Marekani inasikitishwa sana na ripoti za hivi karibuni za mashambulizi dhidi ya waandishi wa habari. Kulinda uhuru na usalama wa vyombo vya habari ni msingi wa demokrasia,” Balozi Meg Whitman alitweet Ijumaa asubuhi.

**BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**CHRISTINA SEVERINE JOSEPH** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0496-0039 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **JITEGEMEE SECONDARY SCHOOL** mwaka 2017. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA:DAR/MBA/RB/115776/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MESHAKI CHARLES** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0145/0521/2020** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **NYAKATO SECONDARY SCHOOL** mwaka 2020. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: MAN/HAY/RB/318799**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI**
**Mkoa D'SALAAM**
**Usimamizi wa mirathi na 524 /2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU TAUSI ABDALLAH SEKE WA......**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA**
**MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA MWANAIDI RAMADHANI MZARA**

### TANGAZO

**( Kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote wowote/ maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wnaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 02 mwezi 05 mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo

**Zingatia**
Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa
**Imetolewa leo tarehe 30 mwezi 03 mwaka 2023**

HAKIMU

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JUSTUS MBERWA BASHARA,** Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **ISUZU BIGHORN** yenye namba za usajili **T378AUQ.** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa Kituo chochote cha Polisi.
Taarifa ya Polisi:
**DOD/DOD/RB/114937/2023.**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**LILILOKO DODOMA**
**MAOMBI NA. 106 YA 2023**
**GEORGE SEULE ........................................MDAI**
**VERSUS**
**PETRO ALEX ........................................MDAIWA 1**
**DAMIANI MLULA ................................ MDAIWA 2**

**KWA:**
**DAMIANI MLULA**
**POPOTE ULIPO.**
**YAH: KUITWA SHAURINI**
Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 25.04. 2023 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
**ANGALIZO:** kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 31 ya mwezi wa MACHI, 2023.

.......................................
MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA.

## KUPOTEA KWA CHETI



**ANNA AKYOO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0672/003 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MKWAKWANI SECONDARY SCHOOL** mwaka **1999.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: IGU/RB/461/201**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SWALEHE IBRAHIM NG'UNGU** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0675/0156** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MBUGWE SECONDARY SCHOOL** mwaka 2019. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/62347/2023**

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 32 OF 2023**

**In the Matter of the Estate of the Late:**
**DANIEL ABEL CHUMA**

**By 1. JOSEPHINE NICHOLAUS BANZILA**
**2. .....................................**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 03 day of 04.2023
Dated at MOROGORO this 28 day of 03..2023

**RESIDENT MAGISTRATE**


**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 0677020701**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**Website: www.ippmedia.com**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa upenuni mwa nyumba moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake. Ilitokea kwenye nyumba moja huko, na mbwa huyo alipouvuta, viungo vya mwili wa binadamu vilianguka. Majirani wa kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Akinamama wakiangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na Muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.

# Maiti kwenye kiroba-2

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

"Tessy ni mfanyabiashara, ana maduka ya nguo Ukonga na Buguruni, huwezi kujua, lakini sidhani kama inaweza kuwa hivyo. Ila nikiri tu siyo kifo cha kawaida, inabidi uchunguzi wa kina ufanyike."

Waandishi wakamuuliza mume wa marehemu, akawajibu kuwa alikuwa amezirai, na sasa fahamu ndiyo zinamrudia, hivyo hawezi kuongea wamuache apumzike.

Wakati amepotea kwa siku hizo tatu mumewe hakuwepo. Mumewe ni mfanyakazi, alikuwa Dodoma, mara nyingi hurejea wikiendi, mume wiki nzima anakuwa Dodoma na mke Dar es Salaam, Ijumaa anarejea, na Jumapili anarudi Dodoma. Unajua alipotoweka siku ile ya kwanza mumewe alikasirika sana, unajua tena mambo ya wivu, lakini siku ya pili akanywea, akaona hii sasa siyo kawaida. Bahati nzuri siku ya pili ilikuwa Ijumaa, akatuagiza tu kwanza tukatoe taarifa polisi, siku ya tatu bado tulikuwa tunahangaika huku na huko, simu yake haipatikani, kila tunapoenda hata kwenye biashara zake hayupo hadi tulipopata hiyo taarifa. Naweza kusema sisi ndugu wa marehemu tumefiwa, lakini aliyepata pigo zaidi ni mumewe. Kwanza ni jinsi alivyoishi kwa amani na mkewe. Aina ya kifo cha mkewe pia kimezidi kumtia simanzi, sijui baada ya hapo ataishi vipi. Tunaomba tu Jeshi la Polisi kufanya kila njia kuwakamata watu hawa."

Maongezi ya mjomba Peter yalichapishwa kwenye magazeti pamoja na kwenye mitandao ya kijamii. Watu wakaendelea kuhuzunika. Wakitaka wauaji watafutwe haraka ili sheria ichukue mkondo wake.

************************************

Inspekta wa Polisi Frank, alikuwa amekaa kwenye kiti chake kikubwa cha kunesanesa ofisini, pembeni kushoto na kulia walikuwa wamekaa wafanyakazi wenzake wenye vyeo vya chini. Koplo Ben na Sajenti Moses. Alikuwa amewatoa ofisi kwake kwa kazi maalum. Aliwaangalia kwa zamu. Jinsi alivyowakodolewa macho, wenyewe walijua kuna kazi nzito kama ilivyo kawaida yake. Ila hawakufahamu ni kazi gani. Hata hawakuwa wanahisi ni nini. Wiki mbili sasa karibuni kila baada ya siku mbili tatu kumekuwa na matukio mbalimbali ya kutisha, ajali na mauaji. Kwa vyovyote vile walijua moja ya tukio watapewa hao ili walifanyie uchunguzi.

"Nimewaita hapa kwa kazi moja tu. Kazi nitakayowapa ni ya kuchunguza au kupeleleza juu ya tukio la kuuawa kikatili kwa mwanamke mfanyabiashara Tessy.




**"Karibu Mgeni." Akamkaribisha akiwa amembeba mtoto wa mmoja wa wapangaji wake.**

Tukumbuke wiki hizi mbili kumefululiza mambo ambayo yamezua taharuki kwa wananchi, sasa imefika wakati wa kuwarejeshea mrejesho. Wanataka kujua kina nani wamefanya haya matukio. Mengine nimewapa maafande wengine, na hili ambalo limesababisha vilio na malalamiko makubwa si kwa wananchi tu, lakini kinamama wameonekana kuguswa sana linahitaji upelelezi wa kina na wa haraka kujua nani amefanya ukatili huu. Nadhani mnanisikia!"

Kwa kawaida kwenye kazi hii mkubwa hapingwi, ila anapewa ushauri tu wa kuboresha kile ambacho amekiainisha.

"Sawa afande." Akaitikia Moses. Ben aliitikia pia, lakini kuna kitu kama kilikuwa kinamtatiza, akamuuliza bosi wake.

"Bosi tunakwenda kuifanya kazi hii, lakini labda kama kuna muongozo wa wapi tuanzie?"

"Upo, ni kwamba mtaanzia pale pale kilipokutwa kiroba cha maiti ya marehemu. Mtaanzia kumhoji mwenye nyumba wa nyumba ambayo kiroba kilikuwa kimeegemezwa kwenye nyumba yake. Baada ya hapo nyumba zinazopakana nayo. Nadhani baada ya hapo kwa uzoefu wa kazi yenu mtakuwa tayari mmeshapata angalau mwanga wa picha nzima ilivyo kabla ya kusonga mbele kumsaka muuaji. Halafu pia nimeongea na askari wengine itakuwa ni kazi ya kwenda Kinondoni Msisiri, kuwakamata vijana wote ambao wanaokota chupa za plastiki kwa ajili ya kuziuza, pamoja na wale ambao wanapita mitaani na kuchukua viroba vya taka kwenye nyumba ili kwenda kuzitupa. Tukumbuke kuwa hawa wanaochukua taka ndiyo hawa hawa ambao huwa wanatelekeza viroba vya taka upenuni au kwenye vichochoro vya nyumba nyingine kama watu hawajawaona. Inaonekana vijana hawa wapo baadhi ambao watakuwa wamefanya uhalifu huu. Tutawachukua, tutawaweka ndani na tuwahoji. Najua kabisa kuwa hatutokosa kitu, Tukiunganisha na maelezo ya wenye nyumba hizo, na wapangaji wao, tunaweza tukawa tupo mbali kwa asilimia nyingi ya jambo hili kubwa." Inspekta Frank aliwapa ramani askari wake ambao walimpigia saluti.

"Haya nendeni, nataka kazi hii muianze kesho asubuhi, msivae unifomu kwa sababu imeshakuwa ni ya kipelelezi zaidi. Hii nyingine ya kuwasomba hao vijana itaanza usiku huu huu." Akamalizia.

***************************************

"We mama Mage wee, njoo umchukue mtoto wako anatupigia kelele hapa, hatusikilizani mimi na mgeni wangu."

Bi. Mkali, mama mwenye nyumba namba 68, Kinondoni Msisiri, akiwa na umri wa miaka 80 sasa. Ni mmiliki wa nyumba hiyo kwa miaka 20 sasa tangu mumewe alipofariki dunia na kumuachia urithi huo. Kwa sasa watoto wake wote hawapo.Wameshaoa na kuolewa. Hata wajukuu zake kwa sasa wameshakuwa watu wazima, nao baadhi wameoa na kuolewa na wengine wako vyuoni.

Vitukuu walikuwa wakija nyakati za likizo na baadaye watakuja kuchukuliwa na wazazi wao. Kwa muda mwingi alikuwa akiishi na wapangaji wake. Bi. Mkali alikuwa kinyume na jina lake. Hakuwa mkali. Badala yake alikuwa mcheshi na mkarimu. Alikuwa na maneno mengi na utani juu.

Saa tatu asubuhi alijiwa na mgeni ambaye hakumfahamu. Kwa sababu anajulikana sana na watu wengi mpaka wengine yeye mwenyewe hawajui, alijua ni mmoja kati ya wale ambao hawamfahamu.

"Karibu Mgeni." Akamkaribisha akiwa amembeba mtoto wa mmoja wa wapangaji wake.

"Ahsante sana bibi shikamoo." Mgeni akamwamkia.

"Marahaba mwanangu, vipi unataka tukae hapa, au tuingie ndani?"

"Nadhani tuingie ndani, itakuwa vizuri zaidi."

Kutokana na ucheshi wake na kupendwa na watu wengi, na utu uzima ulionao, hakuwa na wasiwasi wa kuwa na adui, au mtu yoyote ambaye angeweza kuwa mbaya kwake, hivyo hakuwa na shaka kumuingiza varandani.

Kabla mazungumzo hayajaanza, mtoto akaanza kulia ndipo alipomwita mama yake aende kumchukua.

Mama mtoto alipotoka, Bi. Mkali na mgeni wake wakapeana muda wa kutulia kwanza, kila mmoja akimtazama mwenzake.

Bi.Mkali ndiye alikuwa na maswali zaidi kichwani,"huyu ni nani?"

"Bibi samahani kwa kukuvunjia shughuli zako. Mimi naitwa Sajenti Moses, nimetoka Makao Makuu ya Polisi. Usihofu, nimekuja hapa kwa nia ya kuuliza maswali kadhaa kuhusiana na tukio lililotokea hapa wiki mbili zilizopita la kukutwa na kiroba kilichokuwa na maiti iliyokatwa viungo upenuni mwa nyumba yako."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# SERIKALI KUSAKA WADHAMINI WA LIGI KUU YA WANAWAKE

**Na Saada Akida**

WIZARA ya Utamaduni Sanaa na Michezo imepanga kushirikiana na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), katika mchakato wa kusaka wadhamini mbalimbali kwa ajili ya kusaidia kuinyanyua Ligi Kuu ya Wanawake, imeelezwa.

Lengo ya ushirikiano huo ni kuhakikisha ligi hiyo inatangazwa vyema na kuwavutia wafanyabishara na makampuni mbalimbali kuwekeza.

Hayo yalisemwa katika mkutano wa majadiliano kati ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na wadau wa sekta binafsi yaliyofanyika kwenye Ukumbi wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi.

Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dkt. Pindi Chana, alisema anaamini ushirikiano huo utaiwezesha ligi hiyo kupata wadhamini wengi na hatimaye kuchezwa kwa ufanisi zaidi.

Chana pia, alisema ametoa agizo kwa Naibu wake, Hamis Mwinjuma 'Mwana FA', kufikisha ombi la ongezeko la bajeti katika sekta ya michezo kwa mwaka mpya wa fedha.

Alisema, wizara hiyo imejipanga kuhakikisha maendeleo katika kila sekta iliyopo chini yao inafanya vyema ikiwamo kuwapa nafasi makocha kupata elimu ya juu nje ya nchi ili kuja kufundisha Timu za Taifa pamoja na kutengeneza fursa za kwenda kufundisha nje.

"Tunahitaji kuona Utamaduni na Sanaa nao hawako nyuma kufanya maendeleo katika taifa letu, kufikia huko lazima tuwe na fungu la kutosha, nimemwagiza naibu wangu kupeleka bungeni maombi ya kuongezewa bajeti yetu kwa mwaka huu wa fedha. Tunahakikisha wizara hatui vikwazo vya kukwamisha sekta hii," alisema waziri huyo.

Naye Katibu Mtendaji wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Neema Msitha, alisema inasikitisha Ligi Kuu ya Wanawake inakosa wadhamini wakati katika sekta ya michezo, soka la wanawake ndio linafanya vizuri kimataifa.

Msitha alisema BMT wanaliangalia soka la wanawake kwa jicho la tatu na wanaendelea kushirikiana na TFF ili kuitangaza ligi hiyo kwa kuyashawishi makampuni makubwa kudhamini ligi hiyo.

Aliongeza Ligi Kuu ya Wanawake imekuwa kivutio kikubwa na kwa sasa zinapokutana timu pinzani ( Simba Queens na Yanga Princess), wanaonyesha kandanda safi zaidi ya mpira wa wanaume.

## Mkwawa Queens: Hatushuki daraja

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kuburuza mkia katika msimamo wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, Kocha Mkuu wa Mkwawa Queens, Miraji Fundi, amesema kikosi chake hakitashuka daraja msimu huu kwa sababu kuna mabadiliko makubwa ya kupanda kwa viwango ameyaona kwa wachezaji wake.

Fundi, kocha wa zamani wa Sayari Queens, alisema kikosi chake kimebadilika tofauti na kilivyokuwa katika mechi za mzunguko Kocha huyo alisema timu yake imeimarika na hiyo imeonekana baada ya 'kuzinduka' katika michezo ya mzunguko wa pili iliyoanza.

"Kwa sasa tumeimarika sana, tulianza na timu kubwa, Yanga Princess na Fountain Gate Princess zote ni timu kubwa. Fountain walitufunga mabao mawili lakini kila mmoja aliona utofauti na mzunguko wa kwanza na huu, Yanga princess tumetoka nao suluhu, hii ni kuonyesha sasa wachezaji wameshika mafunzo vizuri," Fundi alisema.

Kuhusu mchezo ujao dhidi ya Amani Queens, kocha huyo alisema wanaendelea kulifanyia kazi eneo la ushambuliaji ambalo kwake anaona ndilo bado lina matatizo.

"Tunawatengeneza, kama kocha naelekeza njia za kufunga lakini hakuna yoyote duniani anaweza kumwambia mchezaji afunge vipi," aliongeza kocha huyo.

Wakati Mkwawa Queens inaburuza mkia ikiwa na pointi mbili, Amani Queens ipo juu yake ikishika nafasi ya tisa na pointi zake nne.



Wachezaji wa timu ya maveterani wakifanya mazoezi ili kujiweka fiti kwenye Uwanja wa Jakaya Kikwete Youth Park, Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Mipango yasukwa Kaskazini Unguja

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MKUU wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohamed, amesema ofisi yake itashirikiana na viongozi wa Chama cha mpira wa miguu mkoani hapa ili kuhakikisha wanapata timu bora zitakazotoa ushindani katika mashindano mbalimbali watakayoshiriki.

Mohamed alisema hayo jana katika kikao kilichohudhuriwa pia na Rais wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Abdul-Latif Ali, kwenye ofisi za kiongozi huyo zilizoko Mkokotoni.

Alisema, anatambua ushindani wa soka uliopo ndani ya mkoa huo dhidi ya timu zinazoshiriki ngazi ya wilaya na anahitaji kuona hamasa inaongezeka.

Alisema timu za Mkoa wa Kaskazini Unguja zimefanya vizuri katika Ligi Daraja la Kwanza Kanda katika msimu huu hali iliyopelekea tata timu moja kutoshuka.

Naye Abdul-Latif alisema wataendelea kushirikiana na viongozi wote kwa ajili ya kutaka kufikia malengo.

"Dhamira yetu ni kuona soka la Zanzibar linakua kuanzia ngazi za wilaya, mikoa na Taifa kwa ujumla ili kupata vijana na timu zitakazoweza kushindana," alisema kiongozi huyo.

## Mtibwa Sugar yaipania Azam

**Na Shufaa Lyimo**

MABOSI wa Mtibwa Sugar wamesema timu yao imejipanga kuvuna pointi tatu katika mchezo wa hatua ya robo fainali ya Kombe la FA dhidi ya Azam utakaochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Pia, Mtibwa Sugar imetamba itaondoka na ushindi katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya wenyeji wao itakayofanyika Aprili 8, mwaka huu.

Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Salum Mayanga, alisema lengo lake ni kusonga mbele katika mashindano hayo na kujiimarisha kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo itaendelea tena kuanzia wiki ijayo.

"Malengo yangu ni kushiriki mashindano ya kimataifa msimu ujao, tutapambana kuhakikisha tufanya vizuri katika Kombe la FA ili tutimize malengo yetu," Mayanga alisema.

Aliongeza anafahamu mechi hizo zitakuwa ngumu kwa sababu wapinzani wao pia wanahitaji kumaliza msimu kwa heshima lakini akifurahia kuimarika kwa afya ya mlinda mlango wake, Mohamed Makaka.

## ZISIKUPITE

### THAMANI YA MOUNT YATAJWA

CHELSEA inataka kitita cha pauni milioni 70 ili kumuuza kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Mason Mount, mwenye umri wa miaka 24, licha ya kubakia kwa mwaka mmoja wa kwenye mkataba wake. ***(Athletic)***

### BARRY KUTUA BAYERN

MABINGWA wa Ligi Kuu Ujerumani, Bayern Munich wanakaribia kukamilisha dili la kumchukua Kocha Msaidizi wa Chelsea, Anthony Barry. ***(90Min)***

### MESSI MSHAHARA MNONO

KLABU ya Al Hilal ya nchini Saudi Arabia inataka kumfanya mshambuliaji wa Paris St-Germain na Timu ya Taifa ya Argentina, Lionel Messi, mwenye umri wa miaka 35, kuwa mchezaji anayelipwa fedha nyingi zaidi duniani. ***(Mirror)***

### MESSI ATAJWA MIAMI

KLABU ya Ligi Kuu Soka ya Marekani, Inter Miami ina matumaini ya kumsajili mshambuliaji wa PSG, Lionel Messi, na kiungo wa kati wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Hispania, Sergio Busquets, mwenye umri wa miaka 34 katika msimu ujao. ***(Sport)***

### UNITED YAKOMAA NA KANE

MSHAMBULIAJI wa Tottenham Hotspur na Timu ya Taifa ya England, Harry Kane, mwenye umri wa miaka 29 anasakwa na Manchester United, hata hivyo mshambuliaji wa Ajax, Mohammed Kudus (22) na mchezaji wa kimataifa wa Ureno anayeichezea Benfica, Goncalo Ramos (21) ni miongoni mwa chaguzi zao nyingine. ***(Manchester Evening News)***

### DE JONG AKARIBIA UNITED

MATUMAINI ya Manchester United ya kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Frenkie de Jong, mwenye umri wa miaka 25 yameongezeka baada ya Barcelona kutaka kumnunua kiungo wa kati wa Manchester City na Ujerumani, Ilkay Gundogan (32). ***(Mirror)***

### WAKALA WA GUNDOGAN AFUNGUKA

WAKALA wa kiungo wa Ujerumani, Ilkay Gundogan amekanusha kuwa nahodha huyo wa Manchester City ameshafanya uamuzi kuhusu mustakabali wake, ingawa yuko tayari kuhama. ***(Guardian)***

### MOYES MAMBO MABAYA

KLABU ya West Ham huenda ikaachana na Kocha, David Moyes, mwishoni mwa msimu huu, bila kujali kama klabu hiyo itaepuka kushushwa daraja. ***(90Min)***

### VIEIRA ATAJWA LEEDS

LEEDS United inaweza kumgeukia kocha wa zamani wa Crystal Palace, Patrick Vieira, katika majira ya joto, ikiwa bosi wa Hispania, Javi Gracia - aliyeteuliwa kama mrithi wa Jesse Marsch hadi mwisho wa msimu ataondoka. ***(TalkSPORT)***

### LAPORTE KUTUA PSG

MLINZI wa Manchester City na Timu ya Taifa ya Hispania, Aymeric Laporte, mwenye umri wa miaka 28 analengwa na Paris St-Germain ya Ufaransa. ***(Football Insider)***

### BASTONI ATAKIWA SPURS

CHELSEA na Tottenham Hotspur wako tayari kupambana kumsajili beki wa Inter Milan na Timu ya Taifa ya Italia, Alessandro Bastoni, mwenye umri wa miaka 23, katika msimu huu wa joto. ***(Fichajes)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# DE GEA: KWA SASA SIFIKIRII MKATABA

**Aeleza kipaumbele chake ni kusaka matokeo mazuri na anafurahia...**

**MANCHESTER, England**

DAVID de Gea ameridhika na Manchester United na anaangalia zaidi kuwasaidia Mashetani Wekundu hao kufuzu kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku mazungumzo kuhusu mkataba mpya wa golikipa huyo yakiendelea.

Mkataba wa De Gea na United unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu huu, ingawa raia huyo wa Hispania amerudia kueleza matumaini yake ataongeza muda wake wa kukaa hapo Old Trafford, akiwa tayari amekaa kwa miaka 12.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 alielezea nia yake ya kumaliza soka yake United mapema mwaka huu, ingawa ripoti kutoka The Athletic wiki hii ilidokeza amekataa ofa ya kwanza ya klabu hiyo ya kutaka kumwongezea mkataba mpya.

Ingawa ripoti hiyo ilipendekeza matokeo chanya bado yanawezekana, De Gea ameweka wazi kuhusu mustakabali wake, huku United ikitarajia kuzishinda Tottenham, Newcastle United na Liverpool kumaliza katika nafasi nne za juu katika Ligi Kuu England.

"Nimekuwa hapa kwa miaka mingi, nikifurahia kila wakati katika klabu hii na kucheza michezo mingi," alisema De Gea akiiambia Sky Sports.

"Bila shaka ni furaha kuwa hapa, na klabu kubwa. Naipenda klabu na nina furaha sana.

Imekuwa hivyo kwa miaka mingi. Kuna kelele nyingi kuhusu kila kitu katika klabu hii, lakini wachezaji wanazingatia tu michezo, hasa ile tuliyo nayo, ni mikubwa kwetu kwa sababu tunataka kumaliza kwenye nne bora.

Tuna michezo mingi kwa hiyo nadhani lazima tujali sana mazoezi, kupona vizuri, kusaidia timu na hilo ndilo jambo muhimu zaidi, zaidi ya mikataba au kitu chochote."

United itacheza na Newcastle United kesho, huku Magpies hao walio katika nafasi ya tano wakipitwa pointi tatu na timu hiyo ya Erik ten Hag iliyopo nafasi ya tatu.

United wameshinda mechi nyingi za Ligi Kuu England ugenini dhidi ya Newcastle kuliko dhidi ya timu nyingine yoyote (14), ingawa wamepoteza mara mbili kati ya tano za mwisho walizocheza kwenye Uwanja wa St James' Park (W2 D1).

## HABARI MICHEZO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,096,0

MECHI KALI
MANCHESTER CITY
VERSUS
LIVERPOOL
1 | 1.64
X | 3.77
2 | 4.68

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ROBERTSON AWAONYA WACHEZAJI LIVERPOOL



**LIVERPOOL, England**

ANDREW Robertson amewaonya wachezaji wenzake wa Liverpool kuwa hawawezi kumudu kufanya makosa yoyote zaidi ikiwa wanataka kufikia matarajio yao ya kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Wekundu hao wamekuwa na msimu mgumu, huku juhudi za Kocha, Jurgen Klopp, zikishindwa kusaidia kutokana na msururu wa majeraha makubwa ya wachezaji muhimu.

Msimu uliopita, Liverpool walishinda Kombe la EFL na Kombe la FA, walifika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, na walimaliza kwa pointi moja tu nyuma ya washindi wa Ligi Kuu England, Manchester City.

Hata hivyo, msimu huu umewafanya washindwe kutetea taji lolote, waliondolewa katika Ligi ya Mabingwa Ulaya katika hatua ya 16 bora na wanakabiliwa na vita ya kumaliza ndani ya nne bora.

Liverpool walio katika nafasi ya sita wamepitwa pointi saba na Tottenham Hotspur iliyopo katika nafasi ya nne, ingawa Wekundu hao wana mechi mbili mkononi.

Hali mbaya ya msimu wa Liverpool haijapotea kwa Robertson, ambaye anadhani wako katika nafasi ya kuzishinda Spurs na Newcastle, na sasa wanakabiliwa na mechi mfululizo dhidi ya City, Chelsea na Arsenal.

"Motisha ni sawa kabisa," alisema akiwaambia waandishi wa habari kabla ya mchezo wa leo Jumamosi dhidi ya City.

Tunataka kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya, na kwa hiyo motisha ni sawa na kwamba tulikuwa tunatafuta mataji."

# Gundogan bado kizungumkuti

**MANCHESTER, England**

HATIMA ya Ilkay Gundogan bado ipo "wazi" licha ya ripoti kudai kiungo huyo wa Manchester City anataka kujiunga na Barcelona baada ya kumalizika kwa mkataba wake, kwa mujibu wa wakala.

Gundogan, anaingia miezi mitatu ya mwisho ya mkataba wa miaka minne aliotiasaini mwaka 2019, na mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani bado hajakubali masharti mapya.

Gundogan amecheza mechi 24 kati ya 27 za Ligi Kuu England msimu huu, lakini ripoti zinadai ana nia ya kuhamia Camp Nou mwishoni mwa msimu huu.



Licha ya mapendekezo Barcelona wako tayari kumpa Gundogan mkataba wa miaka miwili, wakala wa mchezaji huyo na mjomba wake, Ilhan Gundogan, amesema hakuna kilichoamuliwa.

"Hakika hakuna makubaliano bado na klabu yoyote," alisema akiiambia The Guardian.

"Lengo la Ilkay katika wiki za hivi karibuni lilikuwa tu kwa Manchester City na kuzaliwa kwa mtoto wake wa kiume.

"Sasa yuko katika awamu ya mwisho na muhimu ya msimu na anaangazia hilo kabisa. Wapi Ilkay atacheza msimu ujao bado iko wazi."

HABARI MICHEZO

# 041,286/-

# MJASIRIAMALI TABATA ALAMBA KITITA JACKPOT YA SPORTPESA

**Na Mwandishi Wetu**




MKAZI wa Tabata Kimanga, Deus Msigwa, amebahatika kushinda kitita cha Sh milioni 5.6 baada ya kupatia kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya mechi 13, kama bonus ya Jackpot ya SportPesa.

Akizungumza katika ofisi za SportPesa, Oyesterbay Jijini, Dar es Salaam, Deus, anasema alianza kucheza SportPesa miaka miwili iliyopita, baada ya mshikaji wake wake wa karibu, Ezra kushinda Sh. milioni 31 za Jackpot Bonus.

"Mimi nilianza kucheza na SportPesa kama miaka miwili iliyopita. Si kwamba ni mgeni wa michezo hii kabla sijaanza kucheza na SportPesa bali wakati ule nilikuwa nacheza na kampuni nyingine. Sasa kuna mambo hayakwenda sawa, hivyo niliacha kwa muda.

Ilipotokea jamaa yangu Ezra ameshinda Sh. milioni 31, nilianza kuifutailia SportPesa kupitia mitandao ya kijamii na baada ya muda nilipakua app yao na kuanza kujifunza taratibu taratibu namna ya kucheza," alisema Deus.

Aliongeza tangu ameanza kucheza na SportPesa kiwango cha juu kuwahi kula ni Sh. 3,000 kwenye mechi za kawaida ambazo tayari ameshacheza. Kuhusu mkeka huu wa Jackpot ya kati kati ya wiki ulioshinda, Deus alisema, kwa kawaida yeye huwa anaweka mikeka sita ya Jackpot za SportPesa, kila wiki. Huwa naanza na mikeka 3 ya Jackpot ya kati kati ya wiki na pia pale mikeka ya Supa Jackpot inapotoka huwa naweka mikeka mingine mitatu.

Kwa mkeka huu wa ushindi niliweka mkeka siku ya Jumatatu, ambapo baada ya kuziona mechi nilichukua masaa kadhaa kabla ya kuuweka na kusubiria matokeo. Kwa namna ambavyo niko na presha, nikisha weka mkeka huwa siangalii au sifuatilii matokeo.

"Matokeo ya Jackpot bonus hii mimi wala sikuyafuatilia, sasa nilijuaje kama nimeshinda. Nilikuwa zangu kwenye mishe mishe zangu, nakumbuka, ilikuwa majira ya saa 5 asubuhi, nikiwa nafanya mitikasi yangu ikaingia sms ikinipa Hongera.

Nashukuru Mungu juhudi zangu japo kwa kiwango hichi zimefanya kazi na nimeweza kushinda za Jackpot bonus.

Kwa sasa najipanga kuona nitafanyia nini fedha hii, lakini kitu cha kwanza ambacho hakina mjadala ni kupeleka fedha hii kwenye matengenezo ya nyumba yangu ambayo ujenzi bado unaendelea.

Akimalizia Deus anawashukuru SportPesa kwa fursa ya Jackpot bonus kwani ni SportPesa pekee ambapo mchezaji anashinda hela tena nyingi hata kama hakushinda Jackpot yenyewe. "Lazima niwe mkweli katika kutoa shukrani zangu.

Jukumu letu ni moja tu, Kuweka pesa nakucheza!

Akimpongeza Deus kwa ushindi wa Jackpot Bonus ya katikati ya wiki, Mkuu wa kitengo cha mawasiliano SportPesa Sabrina Msuya aliwataka watanzania kuendelea kuiunga mkono SportPesa, kutokana na fursa ambazo zipo kwa wachezaji.

Nafikiri mtakuwa mnakumbuka wiki iliyopita alipatikana mshindi wa Supa Jackpot bonus wa Mil 56, ambaye anatokea Bagamoyo. Leo nipo hapa kumpongeza Deus kwa ushindi wake alioupata baada ya kupatia mechi 12 kati ya 13 kwa usahihi.

Ni juhudi yako kama mchezaji, kuendelea kucheza kila Jackpot zinapotoka, ili uweze kucheza na kujaribu fursa ya kuwa bilionea au milionea kama Deus alivyojishindia mkwanja huu wa Sh 5,615,992.

Supa Jackpot ya wiki kuanzia 13 hadi 17 imesimamia shilingi 1,096,041,286 .

# Simba kurejea Ligi Kuu kitemi

INATOKA UK. 24

tukifanya hivyo, hakika tutakaribia au tutatimiza malengo yetu, bado ubingwa wa ligi uko wazi, tunahitaji kushinda mechi ya FA ili tusonge mbele, lakini kuna mchezo wa robo fainali Afrika, mechi zote hizi tunatakiwa kupata matokeo bora," alisema Mgunda.

Aliongeza kurejea kwa nyota waliokuwa majeruhi, kumeongeza nguvu hasa wakati huu ambao kila timu inahitaji kupata ushindi na kujiimarisha katika msimamo.

"Hakuna mechi rahisi, hakuna mteremko, kila timu sasa inashuka uwanjani ikiwa na malengo yake, walioko juu wanataka ubingwa na walioko chini pia wanahitaji kujinasua, tofauti ya pointi ni ndogo, hivyo lolote linaweza kutokea," kocha huyo wa zamani wa Coastal Union ya Tanga alisema.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba yenye pointi 57 iko katika nafasi ya pili nyuma ya mabingwa watetezi Yanga wenye pointi 65 huku Polisi Tanzania yenye pointi 19 ikiburuza mkia.


## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 01/04/23 | 17:00 | AFC Bournemouth vs Fulham FC | 2.45 | 3.10 | 2.80 |
| 02. 01/04/23 | 17:00 | Crystal Palace vs Leicester City | 2.46 | 3.10 | 2.75 |
| 03. 01/04/23 | 17:00 | Nottingham Forest vs Wolverhampton Wanderers | 2.85 | 3.00 | 2.45 |
| 04. 01/04/23 | 19:30 | Cadiz CF vs Sevilla FC | 3.05 | 3.00 | 2.33 |
| 05. 01/04/23 | 21:00 | SC Cambuur vs FC Emmen | 2.30 | 3.15 | 2.95 |
| 06. 01/04/23 | 22:00 | RKC Waalwijk vs Vitesse Arnhem | 2.55 | 3.25 | 2.60 |
| 07. 01/04/23 | 22:00 | Stade Rennes vs RC Lens | 2.36 | 3.25 | 2.80 |
| 08. 02/04/23 | 13:30 | Bologna FC vs Udinese Calcio | 2.23 | 3.15 | 3.10 |
| 09. 02/04/23 | 13:30 | Umraniyespor vs Konyaspor | 2.90 | 3.50 | 2.24 |
| 10. 02/04/23 | 15:15 | Grasshopper Club Zurich vs FC Lugano | 2.47 | 3.15 | 2.41 |
| 11. 02/04/23 | 16:00 | FC Nantes vs Stade Reims | 2.90 | 3.20 | 2.33 |
| 12. 02/04/23 | 16:00 | Stade Brest 29 vs Toulouse FC | 2.80 | 3.30 | 2.34 |
| 13. 02/04/23 | 16:00 | Giresunspor vs Alanyaspor | 2.33 | 3.20 | 2.50 |
| 14. 02/04/23 | 17:30 | Maritimo Madeira vs Boavista Porto | 2.55 | 3.10 | 2.70 |
| 15. 02/04/23 | 18:30 | Newcastle United vs Manchester United | 2.39 | 3.20 | 2.80 |
| 16. 02/04/23 | 18:30 | Werder Bremen vs TSG Hoffenheim | 2.23 | 3.45 | 2.85 |
| 17. 02/04/23 | 19:30 | Villarreal CF vs Real Sociedad San Sebastian | 2.28 | 3.05 | 3.10 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMAMOSI - 01/04/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 5646 | Manchester City vs Liverpool | 1.64 | 3.77 | 4.68 |
| 15:00 | 3283 | Girona vs Espanyol | 1.90 | 3.30 | 3.85 |
| 16:00 | 1376 | Richards Bay FC vs Orlando Pirates | 3.35 | 2.99 | 2.19 |
| 16:00 | 1576 | Cremonese vs Atalanta | 4.89 | 3.74 | 1.62 |
| 16:00 | 3384 | Trabzonspor vs Kayserispor | 1.49 | 4.20 | 5.67 |
| 16:30 | 1059 | RB Leipzig vs Mainz | 1.48 | 4.31 | 5.42 |
| 16:30 | 1115 | Union Berlin vs Stuttgart | 2.01 | 3.19 | 3.58 |
| 16:30 | 2730 | VfL Wolfsburg vs Augsburg | 1.58 | 3.95 | 4.90 |
| 16:30 | 3444 | Schalke 04 vs Bayer Leverkusen | 3.65 | 3.55 | 1.87 |
| 16:30 | 3982 | Spartak Moscow vs Akhmat Grozny | 1.56 | 4.08 | 4.92 |
| 16:30 | 5268 | SC Freiburg vs Hertha BSC | 1.61 | 3.79 | 4.89 |
| 17:00 | 2299 | West Bromwich vs Millwall | 1.85 | 3.39 | 3.94 |
| 17:00 | 3054 | Nottingham vs Wolverhampton | 2.85 | 2.95 | 2.49 |
| 17:00 | 3133 | Coventry vs Stoke City | 2.30 | 3.21 | 2.91 |
| 17:00 | 3173 | Bournemouth vs Fulham | 2.47 | 3.10 | 2.75 |
| 17:00 | 3721 | Hibernian vs Motherwell | 1.79 | 3.52 | 4.12 |
| 17:00 | 3773 | Crystal Palace vs Leicester | 2.44 | 3.10 | 2.80 |
| 17:00 | 4114 | Kilmarnock vs Hearts | 2.86 | 3.36 | 2.29 |
| 17:00 | 4151 | Cardiff vs Swansea | 2.41 | 3.07 | 2.86 |
| 17:00 | 4518 | Bristol City vs Reading | 1.77 | 3.40 | 4.31 |
| 17:00 | 4608 | Arsenal vs Leeds | 1.31 | 4.96 | 7.90 |
| 17:00 | 4645 | Rangers vs Dundee Utd | 1.11 | 7.82 | 17.05 |
| 17:00 | 4652 | Wigan vs QPR | 2.34 | 3.10 | 2.95 |
| 17:00 | 5264 | Brighton vs Brentford | 1.63 | 3.80 | 4.70 |
| 17:00 | 5338 | St Johnstone vs Aberdeen | 2.88 | 3.13 | 2.39 |
| 17:00 | 5405 | Norwich City vs Sheffield Utd | 2.42 | 3.20 | 2.75 |
| 17:00 | 5609 | Huddersfield vs Middlesbrough | 4.49 | 3.59 | 1.70 |
| 17:15 | 2155 | Athletic Bilbao vs Getafe | 1.57 | 3.55 | 5.81 |
| 17:30 | 4234 | FC Vizela vs Casa Pia Atletico | 2.19 | 3.06 | 3.31 |
| 18:00 | 3484 | AJ Auxerre vs Troyes | 1.85 | 3.39 | 3.94 |
| 18:00 | 4143 | Shirak Gyumri vs Van Yerevan | 2.59 | 2.91 | 2.70 |
| 18:30 | 1764 | Chippa Utd vs SuperSport Utd | 3.77 | 3.09 | 2.00 |
| 18:30 | 1964 | Kaizer Chiefs vs Stellenbosch | 1.97 | 3.19 | 3.71 |
| 18:30 | 5276 | ND Gorica vs Maribor | 4.07 | 3.50 | 1.73 |
| 18:30 | 5479 | Djurgardens IF vs Brommapojkarna | 1.23 | 5.31 | 9.40 |
| 19:00 | 1451 | Inter vs Fiorentina | 1.71 | 3.65 | 4.31 |
| 19:00 | 3328 | Zenit St Petersburg vs Ural Yekaterinburg | 1.31 | 5.01 | 7.72 |
| 19:00 | 3499 | Red Star Belgrade vs FK Mladost Gat | 1.09 | 7.40 | 17.48 |
| 19:30 | 3921 | Cadiz CF vs Sevilla FC | 3.15 | 3.00 | 2.28 |
| 19:30 | 4394 | Chelsea vs Aston Villa | 1.63 | 3.66 | 4.91 |
| 19:30 | 5514 | Bayern Munchen vs Borussia Dortmund | 1.50 | 4.61 | 4.89 |
| 19:45 | 4279 | SBV Excelsior vs Twente | 5.02 | 4.11 | 1.54 |
| 20:30 | 3029 | Samsunspor vs Pendikspor | 1.75 | 3.49 | 3.95 |
| 20:30 | 5632 | Budapest Honved vs Paksi FC | 2.26 | 3.48 | 2.70 |
| 21:00 | 2041 | Amazulu vs Moroka Swallows FC | 2.04 | 2.97 | 3.81 |
| 21:00 | 3431 | Cambuur vs Emmen | 2.30 | 3.15 | 2.95 |
| 21:00 | 3514 | Al Wasl Dubai vs Jazira Abu Dhabi | 2.34 | 3.33 | 2.62 |
| 21:45 | 2352 | Juventus vs Verona | 1.45 | 3.84 | 7.13 |
| 22:00 | 1278 | Elche vs Barcelona | 7.59 | 4.45 | 1.36 |
| 22:00 | 4935 | Rennes vs Lens | 2.45 | 3.30 | 2.65 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumamosi Aprili 1, 2023
Nipashe



UKURASA 21

## De Gea: Kwa sasa sifikirii mkataba

# YANGA YAAHIDI FURAHA CONGO

●●●Mayele asema anataka kutimiza ndoto ya kutetema katika ardhi mama...

**Na Saada Akida**

AKIWA na kumbukumbu ya ushindi katika mechi yao ya kwanza ya hatua ya makundi, mshambuliaji Mkongomani, Fiston Mayele, amewahakikishia furaha mashabiki wa timu hiyo kwa sababu amejiandaa 'kutetema' ili atimize ndoto za kuifungia Yanga mabao akiwa kwenye ardhi ya nyumbani kwao.

TP Mazembe itaikaribisha Yanga katika mechi ya kukamilisha ratiba ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa kesho mjini Lubumbashi, DRC.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mayele, alisema licha ya Congo ni nyumbani kwao, lakini kazi iliyompeleka ni moja ambayo ni kuitumikia Yanga na kufikia malengo ya kuvuna alama tatu muhimu.

Mayele alisema wanahitaji kupata ushindi katika mechi hiyo na kuonyesha ubora wa kikosi chao pamoja na kumfurahisha mdhamini wao Gharib Said (GSM) ambaye ameambatana na timu huko Lubumbashi.

"Bosi wangu amekuja katika ardhi ya nyumbani kwangu, anahitaji kupata furaha katika mchezo wetu dhidi ya TP Mazembe, timu kubwa kwa hapa Congo lakini Yanga ni kubwa Tanzania, malengo yetu ni kusaka pointi tatu muhimu katika mchezo wetu wa Jumapili.

Sasa tunataka kushinda mechi hii ili kuonyesha ukubwa wa Yanga katika michuano ya kimataifa, nimewaahidi mashabiki kutetema katika uwanja uliopo nyumbani kwangu" alisema mshambuliaji huyo mwenye mabao matatu katika hatua ya makundi.

Aliongeza benchi la ufundi limefanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika mechi iliyopita na sasa kazi kubwa imebaki kwa wachezaji kupambana kutafuta matokeo chanya ili kumaliza wakiwa kinara kwenye kundi lao.

Naye Meneja wa Yanga, Walter Harryson, aliliambia gazeti hili kikosi chao kiko vizuri na wamekwenda Congo kwa lengo la kusaka ushindi.



Wachezaji wa Yanga, Dickson Job (kushoto) na Denis Nkane, wakiwa kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere, Dar es Salaam saa chache kabla ya kuelekea Lubumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), kwa ajili ya mechi ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa kesho. **PICHA: MTANDAO**

Meneja huyo alisema maandalizi yote kuelekea mchezo huo yanakwenda vyema na wao wanatambua umuhimu wa kupata pointi tatu na hatimaye kujiweka imara kwa hatua inayofuata.

"Kikosi kiko katika hali nzuri kuhakikisha tunapata pointi tatu na kujiweka kwenye nafasi nzuri kuelekea hatua ya robo fainali, mchezo huu tunauhitaji kwa malengo makubwa, tunajua na tunatambua mashabiki wetu wanaosafiri na walioko hapa Congo wanahitaji ushindi," alisema meneja huyo.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, ametamba kikosi chao kiko kamili kusaka ushindi na kuendeleza shangwe lao la kufanya vyema kwenye mashindano ya kimataifa.

Kamwe alisema wanajisikia fahari kuona timu yao imepata mafanikio makubwa katika msimu huu.

"Tunaongoza katika hatua ya makundi, tunaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, tumefuzu hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika," alitamba Kamwe.

Yanga inaongoza katika msimamo wa Kundi D ikiwa na pointi 10 sawa na US Monastir ya Tunisia, Real Bamako ya Mali inashika nafasi ya tatu ikiwa na pointi tano wakati mabingwa hao wa zamani wa Afrika, TP Mazembe wanaburuta mkia wakiwa na pointi tatu.

Baada ya kumaliza mechi hiyo, Yanga itarejea nyumbani kujiandaa kuwakaribisha Geita Gold FC kwa ajili ya mechi ya hatua ya robo fainali ya michuano ya Kombe la FA itakayochezwa Aprili 8, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

# Simba kurejea Ligi Kuu kitemi

**Na Mwandishi Wetu**

HATUPOI, hayo ni maneno ya Wekundu wa Msimbazi kuelekea lala salama ya Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kumaliza michezo ya hatua ya makundi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, imefahamika.

Joto la kwanza la kimataifa kutoka kwa Simba linawavaa Ihefu FC, katika mechi ya michuano ya Kombe la FA itakayochezwa Aprili 7, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Siku tatu baadaye, Ihefu itaikaribisha Simba katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaofanyika kwenye Uwanja wa Highlands Estates ulioko Mbarali, Mbeya.

Kocha Msaidizi wa Simba, Juma Mgunda, amesema kikosi chao kimeendelea kuimarika kutokana na ushindani waliokutana nao katika michezo mbalimbali ya kimataifa na Ligi Kuu Bara waliyocheza.

Mgunda alisema wamejipanga kuvuna pointi tatu katika kila mechi watakayocheza na wanaamini bado mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Bara ziko wazi kwa sababu idadi ya mechi zilizobakia ni nyingi.

Kocha huyo alisema wakifanikiwa kupata ushindi katika mechi zilizosalia, watakuwa wamejiweka katika nafasi nzuri na hawataki kuangaliwa wapinzani wao wanafanya nini.

"Tunahitaji kupambana ili kuvuna pointi tatu katika kila mechi tunayocheza,

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002